
**Rais Samia alivyodhamiria kuipeleka bandari next level** Uk. 14



**EWURA ilivyoimarisha utoaji huduma za mafuta** Uk. 8



**Nyerere na safari ya kudai uhuru** Uk. 18



**Mabalozi wapongeza uokoaji Hanang, waahidi msaada** Uk. 5

Leo yetu ndiyo kesho yetu

# Uelekeo

| ISSN 2953-2787 | Toleo Na. 00041 | Bei Tanzania sh 1,000 | Jumamosi Desemba 9 - 12, 2023 |

BRELA Business Registrations and Licencing Agency
Air Tanzania The wings of Kilimanjaro
ewura Energy and Water Utilities Regulatory Authority
PSSSF Public Service Social Security Fund
TRA Creating a level playing field
TPA Tanzania Ports Authority

## MIAKA 62 YA UHURU

# Kazi inaongea






**CCM na awamu sita za demokrasia imara** Uk. 12

**Appy Skies yaongeza uhuru wa safari za anga** Uk. 3




**Safari ya BRELA kuelekea maboresho ya kidijitali** Uk. 7

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA


MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA



# MIAKA 62 YA UHURU

9 DESEMBA 2023





## SALAMU ZA PONGEZI

*Bodi ya Wakurugenzi, Uongozi na Watumishi wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), tunaungana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Watanzania wote, kuadhimisha **miaka 62** ya Uhuru wa Nchi yetu.*

"AMANI NA UMOJA NI NGUZO YA MAENDELEO YETU"

Air Tanzania
The wings of Kilimanjaro

MIAKA 62 YA UHURU

# Appy Skies yaongeza uhuru wa safari za anga

- **Ni programu Tumizi ya ATCL (Air Tanzania App) inayoongeza uhuru kwa wasafiri wa anga**





MIAKA 62 iliyopita Tanzania ilipata uhuru wake kutoka kwa utawala wa Waingereza. Taifa hili lililopo ukanda wa Afrika Mashariki linasherehekea uhuru wake sanjari na uboreshwaji wa hali ya maisha ya Watanzania katika nyanja za kiuchumi, siasa, elimu, afya na sekta nyingine mbalimbali.

Moja ya sekta inayochagiza maendeleo ya Taifa ni sekta ya uchukuzi ambapo Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) ndio imebeba dhamana adhimu ya kutoa huduma ya usafiri wa anga nchini.

Mpango Maalumu wa Ufufuaji wa ATCL ulianza baada ya miaka 55 ya uhuru ikiwa ni sehemu ya utekelekezaji wa Ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2015 kutokana na umuhimu wake katika kutoa huduma ya usafiri kwa haraka ndani na nje ya nchi.

Serikali ya Awamu ya Sita chini ya jemedari, Dk. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeendelea kuboresha huduma za ndege na kuimarisha miundombinu ya viwanja vya ndege nchini kote.

Mojawapo ya hatua muhimu iliyochukuliwa na Serikali ni kuendeleza ununuzi wa ndege mpya; uwekezaji ambao umeifanya Air Tanzania kuweza kutanua mtandao wake kibiashara. Hadi kufikia Desemba 2023, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imefanikiwa kununua ndege za kisasa za abiria 13 na ndege moja ya mizigo zinazohudumia vituo vya ndani, kanda na kimataifa. Ndege hizo ni B767-300 (1), B787-8 (2), B737Max 9 (1), Q400 (5), Q300 (1) na A220-300 (4).

Ndege ya mizigo B767-300F imekuwa daraja kwa wafanyabiashara na Mashirika ya Umoja wa Mataifa. Kabla ya ujio wa ndege hii, Air Tanzania haikuwa na uwezo wa kusafirisha bidhaa zenye uzito wa zaidi tani 50 kwa mara moja.

Ujio wa ndege hii ni ukombozi kwa sababu ina uwezo wa kubeba bidhaa zenye kuhitaji nafasi kubwa kama vile magari au zenye uhitaji wa kiwango maalumu cha hali ya hewa, mfano dawa pamoja na bidhaa zinazoharibika kwa muda mfupi yaani matunda, mbogamboga, maua, nyama na nyingine mfano wa hizo.

Kuelekea maadhimisho ya miaka 62 ya Uhuru, Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL), imezindua kampeni ya "Appy Skies" na kutangaza punguzo maalumu kwa wateja watakaokata tiketi kupitia Programu Tumizi ya Air Tanzania (Air Tanzania App) kuanzia tarehe Mosi Desemba 2023 hadi tarehe Mosi Januari 2024. Uwepo wa programu hii umeongeza uhuru kwa wasafiri wa anga wanapohitaji kupata huduma za Air Tanzania muda wowote na kwa faragha.



Akizungumza wakati wa uzinduzi wa "Appy Skies" Mkurugenzi Mtendaji wa ATCL Mhandisi Ladislaus Matindi anasema katika kuendana na kasi ya teknolojia, Programu Tumizi ya Air Tanzania (Air Tanzania App) inalenga kurahisisha upatikanaji wa huduma za safari ambapo mteja anaweza kuhifadhi nafasi ya safari, kukata tiketi, kuchagua kiti, kununua kilo za nyongeza, kubadili safari pamoja na kupata taarifa zote muhimu kuhusu safari yake.

Kupitia App hii wateja wamepewa uhuru wa kujiunga moja kwa moja na huduma ya wasafiri wa mara kwa mara (Twiga Miles) ambapo watavuna pointi 3,000 za ukaribisho.

"Air Tanzania tunaposherehekea Miaka 62 ya Uhuru, tunatoa uhuru zaidi wa uchaguzi kwa wateja wetu," anasema Mhandisi Matindi.

Uhuru mwingine unaotolewa na Air Tanzania ni kuhakikisha wateja wa ndege zetu wanaondokana na hofu iwapo watakumbana na changamoto za safari za ndani ya nchi kupitia bima.

Bima hii humlinda mteja dhidi ya upotevu wa mizigo, kifo au ulemavu wa kudumu, upotevu wa mabegi (Checked-in luggage), safari kusogezwa au kufutwa pamoja na huduma nyingine nyingi iwapo mteja amelipia tiketi yake kupitia benki ya NMB.

Matindi anaeleza kuwa, katika kuhakikisha Kampuni hii ya Taifa inajiendesha kwa tija licha ya kununuliwa ndege mpya za kisasa, kujengewa miundombinu inayoifanya kuwa shindani pamoja na kulipiwa madeni ya zamani; Serikali iliamua kuweka Bodi na Menejimenti mpya. Chini ya uongozi huu mpya, wafanyakazi wamejengewa uwezo hadi kuweza kufanya matengenezo ya ndege kwa kiwango cha Check – C.

Uwepo wa wataalamu hao, umewezesha kampuni kufufua Karakana ya Matengenezo ya Ndege ambayo inaleta ahueni kubwa kwa Air Tanzania na Serikali pale inapotengeneza ndege zake ndani ya nchi. Hii inapunguza gharama ambazo zingelipwa nje ya nchi na kunufaisha nchi zenye makampuni hayo badala ya kuchochea uchumi wa Tanzania.

Karakana hii haihudumii ndege za Air Tanzania pekee bali ndege za kampuni mbalimbali, anafafanua Mhandisi Matindi.

Kutokana na uongozi wao thabiti, Air Tanzania imetunukiwa tuzo mbalimbali ndani na nje ya nchi kwa miaka miwili mfululizo. Tuzo hizo ni pamoja na "Presented Financial Statement Award for year 2022" inayotolewa na Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi Hesabu (NBAA), "Africa Most Preferred Domestic Airline of the year 2023" na "Most Preferred International Airline of the Year 2023" inayotolewa na Consumer Choice Awards.

Mbali na tuzo za taasisi, Mwenyekiti wa Bodi ya ATCL, Prof. Neema Mori na Mkurugenzi Mtendaji Mha. Ladislaus Matindi walitunukiwa tuzo binafsi mwaka 2023 kutokana na uwezo wao katika kusimamia Kampuni hii. Tuzo hizo ni "Board Chair of the Year 2023" aliyotunukiwa Profesa Mori inayotolewa na The Top 100 List na "Africa's Most Respected CEOs Award for year 2023" aliyotunukiwa Mhandisi Matindi inayotolewa na The Business Executive.

Tanzania inapoadhimisha miaka 62 ya uhuru, Kampuni ya Ndege Tanzania ni miongoni mwa wanufaika wa mabadiliko na mageuzi makubwa sana katika vipindi tofauti. Miaka 16 baada ya Uhuru wa Tanzania kufuatia kuvunjika kwa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Serikali iliamua kuanzisha Shirika la Ndege Tanzania (ATC).

Hata hivyo, mwaka 2002 iliamua kulibinafsisha kwa kuingia ubia na Shirika la Ndege la Afrika Kusini na kulibadilisha kutoka Shirika la Umma kuwa kampuni ya biashara ya usafiri wa anga. Kutokana na umuhimu wake kwa nchi, Serikali iliamua kufanya mageuzi kwa kuirejesha tena serikalini na kununua hisa zote. Hii ilikuwa mwaka 2006, na miaka kumi baadaye, yaani mwaka 2016 ilianza rasmi kutekeleza Mpango Maalumu wa Ufufuaji wa Kampuni hii.

Kila tarehe 9 Desemba, Air Tanzania huungana na Watanzania katika kusherehekea Siku ya Uhuru ikiwa ni kumbukizi ya mwaka 1961 wakati iliyokuwa Tanganyika ilipotangazwa kuwa nchi huru.

Tanganyika iliamua kujiunga na iliyokuwa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar mnamo mwaka 1964 na kuzaliwa Taifa la Tanzania.

## MIAKA 62 YA UHURU

# Kazi inaongea

**Na Mwandishi Wetu**

KAZI inazungumza, kazi inaonekana na mwenye macho haambiwi tazama. Ndivyo mtu yeyote mwenye maono akituliza akili, akatazama mambo yaliyofanyika tangu tupate uhuru miaka 62 iliyopita na yanayoendelea kufanyika, hataacha kusema.

Katika kipindi hicho, Tanzania imekuwa na mafanikio makubwa takribani katika kila nyanja; uchumi, huduma za kijamii, demokrasia, michezo, haki za binadamu na usawa wa kijinsia na kadhalika.

Nchi yetu imeendelea kuwa na amani, kulinda utamaduni wetu na kulinda Muungano wetu ambao unaendelea kutoa mafunzo makubwa duniani kote kwani wengi wamejaribu kuungana na wengine wanatamani kuungana lakini imeshindikana.

Tangu Rais Dk. Samia Suluhu Hassan aingie madarakani, Machi 19, 2021, ameendeleza miradi yote mikubwa ya kimkakati aliyoikuta pamoja na kuanzisha miradi mingine mipya na kimsingi kazi zake zinazungumza, zinasikika ndani na nje ya nchi.

### BOMBA LA MAFUTA

Moja ya mradi wa kimkakati wa ujenzi wa bomba la mafuta kutoka Hoima nchini Uganda hadi bandari ya Tanga, Tanzania ambao ujenzi wake tayari umekwishaanza.

Ujenzi wa bomba hilo lenye urefu wa kilometa 1,443 unatekelezwa kwa kushirikiana na mashirika yanayohusika na uzalishaji mafuta ya Tanzania na Uganda, na unatarajiwa kukamilika ifikapo mwakani. Ujenzi huo utainufaisha Tanzania kupata gawio la asilimia 60, wakati asilimia iliyosalia 40 ikichukuliwa na Uganda.

Akishuhudia utiaji saini wa mkataba wa makubaliano wa ujenzi wa bomba hilo, Mei, 2021, Rais Samia alisema hana shaka mradi huo utakamilika na hivyo kufungua ukurasa mpya wa uchumi wa mafuta kwa nchi za Afrika.

Alisema iwapo yale yaliyoandikwa kwenye makubaliano ya mradi huo yatatekelezwa kama ilivyoahidiwa, shughuli ya usafirishaji mafuta ng'ambo huenda ikaanza mwaka 2025.

### BOMBA LA GESI ASILIA

Katika kuimarisha uhusiano wa kijamii na kiuchumi na nchi ya Kenya, Rais Samia ambaye alifanya ziara ya siku mbili nchini humo, Mei mwaka 2021, moja kati ya mambo muhimu katika ziara hiyo ilikua utiaji saini mradi wa ujenzi wa wa Bomba la Gesi Asilia kutoka jijini Dar es Salaam kwenda mji wa Mombasa nchini Kenya.

Tanzania inakadiriwa kuwa na futi za ujazo trilioni 57.25 za gesi asilia katika hifadhi za nchi kavu na baharini inayoweza kusaidia Kenya kukidhi mahitaji ya gesi safi kwa matumizi ya nyumbani na viwandani.

Rais Samia alisema utekelezji wa mradi huu utaanza mara moja baada ya kutia saini makubaliano hayo, hivyo kinachofuata ni usimamizi wa utekelezaji wa mradi huo ili uweze kukamilika kwa wakati.

### MRADI WA SGR

Wakati Rais Samia anaingia madarakani, ujenzi wa reli hiyo ya kisasa kuanzia Dar es Salaam hadi Morogoro, kipande cha kilomita 202 ulikuwa asilimia 90, ambapo kipande cha Morogoro hadi Makutupora cha urefu wa kilomita 348 kilikuwa asilimia 50.

Lakini kwa sasa kipande cha Dar es Salaam hadi Morogoro ujenzi wake umekamilika na Morogoro hadi Makutupora umefikia zaidi ya asilimia 82.

### MRADI WA JHPP

Ujenzi wa Bwawa la Umeme la Julius Nyerere ulifikia asilimia 50 wakati Rais Samia alipoingia madarakani, lakini sasa ujenzi wa mradi huo umefikia zaidi ya asilimia 90 ukitarajiwa kukamilika na kuanza kazi kwa majaribio hapo mwakani.

### DARAJA LA JPM

Aidha, Rais Samia ameendelea kuelekeza fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kimkakati ikiwemo ujenzi wa daraja la Magufili katika eneo la Kigongo-Busisi mkoani Mwanza, Daraja hilo muhimu linatazamiwa kukamilika mwaka 2024, likigharimu shilingi bilioni 716.33.

### DARAJA LA TANZANITE

Chini ya uongozi wake, Rais Samia amekamilisha ujenzi wa daraja jipya la Tanzanite lililopo mkoani Dar es Salaam lenye urefu wa kilomita 1.30 na barabara unganishi zenye urefu wa kilomita 5.2 lililogharimu kiasi cha shilingi bilioni 243.

Daraja hili ambalo linapita baharini kuunganisha eneo la Agha Khan pamoja na Coco Beach linajumuisha njia nne za magari pamoja na njia mbili za watembea kwa miguu limepunguza kwa kiasi kikubwa changamoto ya foleni ambayo daraja la zamani la Selander lilizidiwa kutokana na kuongezeka kwa shughuli za kibinadamu katikati ya Jiji la Dar es Salaam.

Ujenzi barabara ya mzunguko wa nje

Mradi wa ujenzi wa barabara ya mzunguko wa nje (Outer Ring Road) yenye urefu wa kilomita 112.3 katika Jiji la Dodoma itakayogharimu Sh. bilioni 249 ambazo ni gharama za ujenzi wa ulipaji fidia kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo tayari ulishafanyika.

Barabara hii ambayo ni kichocheo cha ukuzaji wa uchumi imesanifiwa kuwa na umbali wa kilomita 20 kutoka katikati ya jiji la Dodoma imegawanywa katika sehemu mbili, sehemu ya kwanza inayopita eneo la Veyula – Mtumba hadi Bandari Kavu ya Ihumwa yenye urefu wa kilomita 52.3 na sehemu ya pili inayoanzia Bandari Kavu ya Ihumwa kupitia Matumbulu hadi Nala yenye urefu wa kilimita 60.

### KIWANJA CHA NDEGE MSALATO

Mradi wa ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato mkoani Dodoma, kazi ya ulipaji fidia imekamilika na mkataba wa awamu ya kwanza unaohusisha ujenzi wa barabara ya kuruka na kutua ndege, maegesho ya ndege ulisainiwa Septemba, 2021 na mkandarasi tayari alikabidhiwa eneo la mradi, Januari, 2022.

### MRADI BANDARI YA UVUVI KILWA

Rais Samia alizindua ujenzi wa mradi wa Bandari ya Uvuvi Kilwa katika Mkoa wa Lindi unaojengwa na Kampuni ya Bandari ya China (CHEC) Septemba, 19 mwaka huu.

### UBORESHAJI ATCL

Waziri Mkuu Kassim Majaliwa hivi karibuni aliliambia Bunge kwamba Serikali imetoa Sh bilioni 20.52 kwa ajili ya kuboresha shirika hilo.

Alisema shughuli zilizofanyika ni pamoja na kulipa sehemu ya gharama za ununuzi wa ndege tano ambapo kati ya hizo, ndege moja ni aina ya Boeing 767-300F ya mizigo, ndege mbili aina ya Boeing 737-9, ndege moja aina ya Boeing 787-8 Dreamliner na ndege moja aina ya De Havilland Dash 8-Q400.

### UBORESHAJI TPA

Serikali imeingia mkataba wa miaka 30 na Kampuni ya DP World ya kuendesha Bandari ya Dar es Salaam kwa kuingia mikataba mitatu ya uwekezaji na uendeshaji wa Bandari ya Dar es Salaam, iliyoingiwa na Mkataba wa Nchi Mwenyeji, Mikataba ya Ukodishaji na Uendeshaji wa Gati namba 4 hadi 7.

Aidha, gati namba 0 hadi 3 zitatumiwa kwa pamoja baina ya Kampuni ya DP World na Serikali kupitia TPA kwa ajili ya shughuli zingine za kibiashara na Serikali.

Moja ya faida lukuki ya mkataba huo ni kuongezeka kwa ajira maradufu na mapato ya serikali yatokanayo na kodi ya forodha inayokusanywa katika shehena inayopitishwa bandarini kutoka Shilingi trilioni 7.76 kwa mwaka 2021/22 hadi Shilingi trilioni 26.70 kwa mwaka 2032/33.

### PROGRAMU YA BBT

Rais Samia anataka kuona mabadiliko makubwa kwenye sekta ya mifugo na uvuvi kwa kuona vijana na akina mama wengi wanaingia kwenye sekta hizo ili kujiongezea kipato na kuongeza Pato la Taifa


Katika kuhakikisha hilo linatekelezwa, Rais Samia ameielekeza Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuingia kwenye mpango wa Jenga Kesho iliyo Bora (Building Better Tomorrow - BBT) ambao unawaandaa vijana kwa lengo la kufanya ufugaji na uvuvi kibiashara. Yaani sio tu bora kufuga, kwa wale watakaokuwa wananenepesha ng'ombe kwa lengo la kupeleka viwandani na kuuza sambamba na watakaofuga samaki kwenye vizimba na mabwawa.

### TANZANIA: THE ROYAL TOUR

Filamu hiyo imeleta hamasa na mguso na imeongeza idadi ya watalii na wawekezaji nchini. Tayari serikali imetaja mafanikio yaliyotokana na filamu hiyo ambapo hadi Machi mwaka huu, jumla ya miradi mikubwa 26 ya uwekezaji katika utalii imesajiliwa, ikilinganishwa na miradi 16, Machi 2020.

### MIRADI LUKUKI

Miradi mingine ni Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, Mradi wa Tanzania ya Kidijiti, Mradi wa Mfumo wa Anwani za Makazi na Postikodi, Upanuzi wa Usikivu wa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) na Habari kwa Umma, kusambaza umeme karibu vijiji vyote vya Tanzania, uboreshaji wa tiba zikiwemo za kibingwa na kuifanya Tanzania kuwa nchi ya utalii wa matibabu, uboreshaji wa miradi ya maji na elimu na kadhalika na kadhalika.



# Mabalozi wapongeza uokoaji Hanang, waahidi msaada

**Na Mwandishi Wetu**

MABALOZI na Wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa nchini wamepongeza jitihada zinazochukuliwa na serikali katika zoezi la uokoaji wilayani Hanang baada ya eneo hilo kukumbwa na maporomoko ya tope kutoka Mlima Hanang' kufuatia mvua kubwa iliyonyesha Desemba 2, mwaka huu.

Walitoa pongezi hizo jijini Dar es Salaam jana walipokutana na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, January Makamba, aliyewaita kuwaelezea kilichotokea Hanang mkoani Manyara na hatua zilizochukuliwa na serikali katika kukabiliana na janga hilo.

Makamba alisema maporomoko hayo ya tope yamesababisha vifo vya watu 72, kujeruhi watu 117, kuharibu mali za watu, makazi na miundombinu ya barabara, maji na umeme.

"Serikali ya Tanzania inaishukuru Jumuiya ya Kimataifa nchini kwa jinsi ilivyoikimbilia na kusaidia manusura wa maporomoko hayo hasa katika kusaidia urejeshaji wa huduma muhimu za kibinadamu kwa wananchi wa eneo la Katesh," alisema.

Alisema katika kukabiliana na janga hilo, Serikali iliunda Kamati ya Kitaifa ya Maafa iliyo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu inayoshirikiana na mamlaka ya Mkoa wa Manyara na kufungua akaunti maalumu ya maafa kwa ajili ya kuratibu na upokeaji misaada ili kusaidia manusura wa maporomoko hayo na kuwezesha maisha ya watu kuendelea kama kawaida.

Naye Mwakilishi Mkazi wa Umoja wa Mataifa nchini, Zlatan Milišić, amepongeza hatua za haraka zilizochukuliwa na Serikali katika zoezi la uokoaji wa wananchi na mali zao na kuongeza kuwa Ofisi ya Umoja wa Mataifa Tanzania itaendelea kushirikiana na Serikali.

Alisema mashirika ya Umoja wa Mataifa nchini yameungana na kuchanga misaada yao ya kibinadamu kwa ajili ya kusaidia manusura hao, misaada ambayo wataikabidhi serikalini.

Naye Balozi wa Kenya nchini, Isaac Njenga, alisema Kenya kama nchi jirani iko pamoja na Watanzania katika sala na maombi kuwaombea marehemu na kutoa pole kwa familia za marehemu.

Akizungumza katika kikao hicho Balozi wa Somalia nchini, Zahra Ali



Hassan, alisema Umoja wa Mabalozi wa Afrika kwa umoja wao wameungana na kuwaingiza katika maombi manusura wa maporomoko hayo na kuchanga misaada ya kibinadamu ambayo wataikabidhi kwa serikali na kutoa pole kwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

Kwa upande Balozi wa Msumbiji, Ricardo Mtumbuida, alisema Msumbiji inaungana na Tanzania na kutoa pole kwa Rais, Watanzania na wahanga wote na kuwaombea marehemu wapumzike kwa amani.

# MNH yaitika wito wa Samia msaada Hanang

**Na Mwandishi Wetu**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH) imepeleka msaada wa dawa na vifaa tiba vyenye thamani ya Sh milioni 38 ili kusaidia jitihada za utoaji huduma kufuatia vifo na majeruhi waliotokana na maporomoko ya udongo mjini Katesh wilayani Hanang, Mkoa wa Manyara.

Desemba 2, mwaka huu, eneo la Katesh lilikumbwa na maafa ya maporomoko ya matope kutoka Mlima Hanang na kusababisha madhara ikiwemo vifo, majeruhi pamoja na upotevu wa mali na uharibifu wa miundombinu.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa MNH, Mkuu wa Idara ya Famasi, Mfamasia Nelson Faustine, alisema pamoja na msaada huo, hospitali imetuma Msaikolojia Tiba kwenda kuungana na timu za wataalamu mbalimbali walioko wilayani Hanang wanaotoa huduma kwa waathirika wa mafuriko hayo.

Alisema, hatua hiyo ni kuitikia wito wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ambaye ameagiza kupelekwa wataalamu wa saikolojia kuzungumza na wananchi waliopata mfadhaiko kutokana na tukio hilo ili waweze kurejea katika hali ya kawaida.

**Desemba 2, mwaka huu, eneo la Katesh lilikumbwa na maafa ya maporomoko ya matope kutoka Mlima Hanang na kusababisha madhara ikiwemo vifo, majeruhi pamoja na upotevu wa mali na uharibifu wa miundombinu.**



PONGEZI KWA MIAKA 62 YA UHURU

BODI YA WAKURUGENZI, MENEJIMENTI NA WATUMISHI WA CHUO CHA BAHARI DAR ES SALAAM (DMI) WANAUNGANA NA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN NA WATANZANIA WOTE KATIKA KUADHIMISHA MIAKA 62 YA UHURU WA TANZANIA.

KATIKA KUADHIMISHA MIAKA 62 YA UHURU DMI INAJIVUNIA MAFANIKIO YAFUATAYO;

- Utoaji Elimu kwa wanafunzi kuhusu masuala ya bahari umeongezeka kutoka wanafunzi 2299 (mwaka 2021/22); hadi wanafunzi 3505 (mwaka 2022/23)
- Kuwaunganisha wahitimu na soko la ajira kwenye makampuni ya usafirishaji baharini na makampuni mengine yanayojihusisha na shughuli za bahari duniani;
- Kutoa rasilimali watu yenye weledi kutoka wahitimu 2299 mwaka 2021/23 hadi wahitimu 3505 mwaka 2022/23 wanaotumika katika Wizara, Taasisi za Umma na Binafsi na makampuni yanayo jihusisha na bahari;
- Kutoa elimu ya uchumi wa Buluu kupitia makongamano na machapisho;
- Kutoa ushauri elekezi kwenye masuala ya bahari na usafirishaji kwa njia ya maji.

DMI inaishukuru Serikali kupitia Wizara ya Uchukuzi kwa kuendelea kuiwezesha kutoa mafunzo yenye viwango vya ubora vya kimataifa vya ISO 9001:2015 na kupata mtambo maalum wa kufundishia (Full Crane Simulator) utakaosaidia mafunzo kwa vitendo.



RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN

DMI - KITUO CHA UBORA CHA ELIMU NA MAFUNZO YA BAHARI
"TANZANIA IMARA, KAZI IENDELEE"

# Maoni ya Mhariri & Uchambuzi

## HII NI KERO

### Tuwe tayari kuifia Tanzania

TANZANIA Bara (Tanganyika) leo imetimiza miaka 62 tangu ijikomboe kutoka mikononi mwa wakoloni wa Kiingereza. Baada ya Uhuru huo, Tanganyika ikaungana na Zanzibar na kuzaliwa Tanzania tunayojivunia.

Waswahili wanasema "kimfaacho mtu ni chake" na hivyo kila Mtanzania ana dhima ya kujivunia nchi yake.

Kero kubwa ni kuona baadhi ya Watanzania wakitamani kuzaliwa Ulaya na kudharau nchi yeo. Na wapo ambao hawaonekani kuwa na uzalendo na kuthamini vya kwao ikiwemo mila na tamaduni zetu. Kuna wanasiasa wanafika mbali na kulisema vibaya taifa letu kwa wageni hata mambo ambayo hawajaulizwa.

Ushauri wangu kwa Watanzania wenzangu ni kupenda nchi yetu kwa dhati na kuwa tayari kuifia, na kuitangaza vizuri kila wakati.




## MAONI YA MHARIRI

# Tuimarishe nguzo 4 za Samia tunaposherehekea uhuru

LEO Watanzania tumeungana na waliokuwepo mwaka 1961 ambao waliisubiri kwa hamu siku kama ya leo (usiku wa manane wa kuamkia leo) ili kuona bendera ya Mwingereza, maarufu kama "Union Jack", iliposhushwa usiku wa manane; na bendera ya Tanganyika huru ikapandishwa kuchukua nafasi yake, kuashiria "uhuru kamili" wa Tanganyika.

Katika salamu zake za uhuru, Rais wa Kwanza wa Tanzania, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alisema: "Tunasherehekea ushindi. Lakini tukumbuke kwamba ushindi tuliopata ni ile haki ya kufanya kazi wenyewe, haki ya kupanga na kujenga nchi yetu kwa uhuru, bila kuingiliwa."

Mwalimu alizungumzia pia imani ya Tanu (baadaye CCM) juu ya usawa wa binadamu na heshima kwa wote ambapo alisema: "Tumekubaliana kwamba taifa letu litakuwa la raia huru walio sawa, ambamo kila mmoja atapata fursa kutumia uwezo wake kuendeleza jamii...Hakuna kitu kitakachomwondolea haki ya kazi zake kama mjumbe wa jamii. Na hili lazima tuanze kulitekeleza."

Tangu aingie madarakani Machi 19, 2021, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan amekuwa akijipambanua kama kiongozi anayeongoza kwa kutumia nguzo nne ambazo zinalenga katika kuliunganisha Taifa la Tanzania katika nyanja zote zikiwemo za kisiasa, kijamii, kiuchumi na kiutamaduni kama msimamo aliyokuwa na Mwalimu Nyerere.

Katika kulifanya taifa kuwa moja lenye kufurahiwa na kila Mtanzania, Rais Samia amekuwa akiziweka nguzo hizo nne katika falsafa ya "R" nne, ambazo ni Maridhiano (Reconciliation), Ustahamilivu (Resilience), Mageuzi (Reforms) na Ujenzi Mpya (Rebuild).

Hakuna ubishi kwamba kupitia maridhiano katika nyanja ya siasa ambapo kwa nyakati tofauti amekutana na viongozi wa vyama vya siasa, Rais ameonesha kwamba taifa letu ni la raia huru walio sawa, ambamo kila mmoja anapata fursa kutumia uwezo wake kuendeleza jamii.

Dk. Samia amekuwa akisisitiza umuhimu wa kushirikiana ili kuijenga Tanzania yetu yenye kuaminiana na kuheshimiana kwa misingi ya haki na usawa.

Ni vyema Watanzania wakiwemo walioko kwenye vyama vya siasa kufahamu nia hiyo ya Rais na kumuunga mkono ikiwa ni pamoja na kuendesha siasa za kistaarabu katika kipindi hiki ambacho mikutano ya kisiasa imeruhusiwa. Wajenge hoja zenye kutuleta pamoja kama Watanzania na si kutugawa, au kufanya watu waichukie serikali yao.

Kubwa tuzidi kuchunge amani ya nchi yetu. Tukosoane kwa ustaarabu pale kwenye makosa kwa kuwa nchi haiongozwi na malaika lakini pia tuunge mkono kila jema linalofanywa na viongozi wetu kwa faida ya nchi yetu.


## Wasiliana nasi

**Mhariri Mkuu:** +255713263775 / +255748115000
**Mhariri wa Habari:** +255768411003
**Mhariri Michezo:** +255787559090
**Meneja Masoko/Biashara:** + 255718480406 / + 255733768825
**S. L. P:** 15110, Dar es Salaam
**Makao Makuu Mtaa:** Barabara ya Morogoro
**Jengo la:** Aura Mall
**Chumba Cha Habari:** +255 (0)222151532
**Email:** uelekeohabari@gmail.com





Na Godfrey Sanga
JICHO LANGU
Sangagodfrey26@gmail.com


# Samia anavyopambania kilimo

KILIMO kina maana pana inayojumuisha mifumo ya uzalishaji mimea, ufugaji wa wanyama na uvuvi wa samaki pia. Mara nyingi kilimo cha mimea kinaenda sambamba na ufugaji wa wanyama, lakini leo ngoja tujikite katika kilimo cha mimea.

Kilimo hiki watu hupanda mimea na kuitunza hadi mavuno hasa kwa ajili ya uzalishaji wa chakula na lishe ya wanyama, lakini pia kwa shabaha ya kupata malighafi mbalimbali zinazotumiwa katika viwanda vyetu.

Mbali na kilimo kutuhakikishia chakula, lakini pia ziada huuzwa kibiashara na mazao mengine kama pamba yanalimwa kwa ajili ya biashara moja moja kwa moja.

Kwa mantiki hiyo, mbali na kumwingizia mtu kipato lakini pia kilimo kinachangia katika kukuza uchumi wa nchi.

Inasemekana kuwa watu walianza kulima takriban miaka 10,000 iliyopita na kabla ya hapo watu waliwinda tu na kukusanya matunda.

Tumeshuhudia serikali za wamu zote nchini namna zinavyopambana na kujipambanua katika kuinua kilimo kwa namna mbalimbali na hasa kwa kuzingatia kwamba Watanzania zaidi ya asilimia 60 wanategemea kilimo kama ajira yao.

Serikali ya awamu ya kwanza chini ya uongozi wake Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere ilihamasisha kilimo kwa kaulimbiu mbalimbali ikiwemo ya 'Siasa ni Kilimo' iliyotokana na Azimio la Iringa la mwaka 1972.

Ni azimio lililotaka nchi iboreshe kilimo na kwamba siasa isijitenge na dhima ya kuendeleza kilimo nchini.

Lakini kufuatia njaa iliyoikumba dunia katika miaka 1970, serikali ya Mwalimu Nyerere ilikuja na kaulimbiu nyingine ya 'Kilimo cha Kufa na Kupona' ili kujikinga na balaa la njaa.

Serikali ya Awamu ya Nne iliyoongozwa na Rais Jakaya Mrisho Kikwete ilikuja na kaulimbiu ya 'Kilimo Kwanza', kauli iliyolenga kukitanguliza kilimo mbele na hasa ililenga kuhamasisha sekta binafsi kushirikiana bega kwa bega na serikali katika kukuza kilimo.

Kwa kufahamu umuhimu wa kilimo na mchango wake kwa Watanzania na nchi kwa ujumla, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na na Rais, Dk. Samia Suluhu Hassan imejipanga kunyanyua kilimo ipasavyo.

Moja ya kitu bora kinachofanywa na serikali ya Awamu ya Sita ni Mpango wa "Jenga Kesho iliyo Bora" (Building a Better Tomorrow -BBT).

Mpango huu unalenga kuongeza ushiriki wa vijana wakikwemo wasomi katika kilimo kwa kuwapatia mafunzo, maeneo ya mashamba, mitaji na kuwaunganisha na fursa za masoko.

Mpango huu uliozinduliwa Agosti 3, mwaka jana katika maonesho ya Siku Kuu ya Wakulima (NaneNane) yaliyofanyika kwenye Viwanja vya John Mwakangale Jijini Mbeya umeshaanza kutoa manufaa makubwa.

Lakini Serikali ya Rais Samia imejipanga katika kuongeza skimu za umwagiliaji huku ikitoa mitambo ya kuchimba visima karibu katika wilaya nchini. Pia serikali imeboresha huduma za ugani na vyama vya ushirika kuhakikisha kwamba haina utani katika kukuza kilimo.

**Mpango huu unalenga kuongeza ushiriki wa vijana wakikwemo wasomi katika kilimo kwa kuwapatia mafunzo, maeneo ya mashamba, mitaji na kuwaunganisha na fursa za masoko.**

BRELA
BUSINESS REGISTRATIONS AND LICENCING AGENCY

## MIAKA 62 YA UHURU

# Safari ya BRELA kuelekea maboresho ya kidijitali



**Afisa Mtendaji Mkuu, Godfrey Nyaisa**

**Na Mwandishi Wetu**

'BRELA kidijitali' ni jitihada za kutoa huduma kwa njia ya teknolojia zilizofanywa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) katika kuhakikisha kuwa huduma zote za Wakala zinapatikana kwa njia ya mfumo rahisi na unaopatikana takribani kila mahala.

**SHERIA ILIYOANZISHA BRELA**

Mnamo mwaka 1999, Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) ambao ndio kitovu kikuu cha urasimishaji wa biashara nchini Tanzania ulianza kufanya kazi zake rasmi baada ya kuanzishwa chini ya Sheria ya Wakala za Serikali Na. 30 ya mwaka 1999.

Majukumu ya Wakala yameainishwa katika waraka wa uanzishwaji wake Na. 38 kupitia Tangazo la Serikali. Majukumu hayo ni pamoja na usajili wa kampuni, usajili wa majina ya biashara, usajili wa alama za biashara na huduma, utoaji wa hataza, leseni za viwanda na leseni za biashara daraja A.

**MFUMO WA MAKARATASI**

Huko nyuma, kazi zote kuu za wakala zilikuwa zikifanyika kwenye makaratasi ambapo mteja aliyehitaji huduma inayotolewa na Wakala ilimlazimu kutoka eneo alilopo, bila kujali umbali, na kufuata huduma katika ofisi za Wakala zilizoko Dar es Salaam.

Kipindi hiki kiligubikwa na adha kubwa ambazo walikuwa wanapata wateja kama vile kupoteza muda mrefu kuandaa, kusafirisha na kufuatilia nyaraka mbalimbali za usajili.

Aidha, kipindi hiki kilihusishwa pia na ubabaishaji wa 'vishoka'. Kutokana na adha iliyokuwa inawapata watu waliotaka kusajili biashara zao, walijikuta wakitafuta watu wa kuwasaidia lakini baadhi yao wakaangukia mikononi mwa watu, maarufu kama vishoka, ambao hawakuwa waaminifu.

Gharama za usajili hazikuwa kubwa kwa mujibu wa jedwali la ada za usajili la sheria lakini kutokana na ufuatiliaji na wakati mwingine kutapeliwa na vishoka wateja walijikuta wakiingia gharama kubwa.

**SERIKALI SIKIVU**

Serikali haikuwa mbali. Iliiona hili na kuchukua hatua za makusudi kumsaidia Mtanzania mwenye nia thabiti ya kurasimisha biashara yake.



**Makamu wa Rais Dk. Philip Mpango, akimkabidhi cheti cha Udhamini Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Godfrey Nyaisa kwa kutambua mchango wa taasisi hiyo katika kuwezesha kufanyika kwa mkutano wa 37 wa Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania.**


Mwaka 2018, Wakala ulifanya maboresho makubwa katika utoaji wa huduma kwa wateja wake kwa kuleta mfumo unaofahamika kama BRELA ONLINE REGISTRATION SYSTEM.

Huu ni mfumo unaotumika katika kusajili kampuni, majina ya biashara, alama za biashara, utoaji wa hataza pamoja na leseni za viwanda.

Mfumo huu ulileta mageuzi makubwa nchini kwa kuhakikisha kuwa taarifa zote za mteja zinapatikana kwenye mfumo. Hii ilisababisha pia kampuni zote zilizosajiliwa kabla ya mfumo kuanza kutumika kutakiwa kuhuisha taarifa zao kwenye mfumo ili kuepushwa kufutwa kwenye daftari la makampuni.

Usajili mpya sasa unatakiwa kufanywa kwa njia ya mfumo bila mhusika kulazimika kufika ofisi za Wakala kwa ajili ya usajili. Hivyo, kuanzia mwaka 2018 hadi leo huduma zote za Wakala zinatolewa kwa njia ya mtandao kiasi kwamba mahali popote mteja anaweza kupata huduma yoyote inayotolewa na Wakala alimradi kuwe na mtandao wa kompyuta.

> **Mfumo huu ulileta mageuzi makubwa nchini kwa kuhakikisha kuwa taarifa zote za mteja zinapatikana kwenye mfumo. Hii ilisababisha pia kampuni zote zilizosajiliwa kabla ya mfumo kuanza kutumika kutakiwa kuhuisha...**



**Mwenyekiti Bodi ya Ushauri BRELA akipokea maoni ya wafanyabiashara**

Mfumo huu umeleta manufaa makubwa kwa kuharakisha na kurahisisha upatikanaji wa huduma, kupunguza gharama za usajili, kuondoa adha iliyosababishwa na vishoka, kutoa usaidizi wa kiusajili na upatikanaji wa taarifa kwa haraka. Halikadhalika unasaidia katika kuhifadhi kumbukumbu sahihi za usajili.

**CHANGAMOTO**

Hata hivyo, Wakala umekuwa ukikumbana na changamoto mbalimbali ikiwemo maombi ya wateja kuwasilishwa kwa njia ya mtandao yakiwa na makosa mbalimbali yanayosababisha maombi hayo kushindwa kukamilika.

Kimsingi, hali hii husababishwa na mteja kutokuwa na elimu ya kutosha kuhusiana na huduma za Wakala, elimu ya matumizi ya kompyuta kuwa hafifu kwa wateja wa Wakala, mfumo kutokuwa rafiki zaidi kwa watumiaji na hivyo mteja kutumia muda mrefu mpaka kukamilika.

**MABORESHO ZAIDI**

Pamoja na changamoto hizo, Wakala umeendelea na maboresho kila yanapohitajika ili kuhakikisha mteja anaendelea kupata huduma anayohitaji bila usumbufu wala gharama ya ziada.

Tunapoadhimisha miaka 62 ya uhuru, Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni BRELA anajivunia kutekeleza majukumu yake yote kwa njia ya mtandao, hali ambayo sasa haileti mashaka yoyote mtu kutamka BRELA KIDIJITALI

Hii ina maana kwamba BRELA sasa inakwenda na wakati na kisasa kwa kuwezesha shughuli zake za usajili, utoaji wa leseni, na utoaji wa taarifa mbalimbali kwa wadau na wateja kufanywa kielektroniki.

MIAKA 62 YA UHURU

ewura
Energy and Water Utilities Regulatory Authority



# EWURA ilivyoimarisha utoaji huduma za mafuta nchini

Na Mwandishi Wetu

HEBU jaribu kufumba macho na kufikiria kama kusingekuwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) hali ingekuwaje katika nchi yetu ambayo leo inaadhimisha miaka 62 tangu ipate uhuru wake?

Jibu la haraka ni kwamba maslahi ya watumiaji wa bidhaa hizo muhimu, hususani nishati ya mafuta ambayo makala haya yanaangazia zaidi, yasingelindwa ipasavyo. Kungekuwa na mfumuko wa bei na uchakachuaji wa mafuta kwa ajili ya magari na mitambo ungekuwa juu.

Hata hivyo, ukisoma makala haya hadi mwisho utagundua kwamba EWURA iliyoanzishwa mwaka 2012 kwa Sheria ya Mamlaka ya Huduma za Nishati ya mwaka 2001, Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania, ina majukumu mengi muhimu ambayo yanafanya huduma ya nishati ya mafuta nchini kuwa nzuri muda wote.

## MAJUKUMU YA EWURA

Kwa mujibu wa vyanzo mbalimbali, baadhi ya majukumu ya mamlaka hiyo ni kudhibiti huduma za mafuta na maji, kudhibiti shughuli za mkondo wa kati na wa chini unaohusisha mafuta na gesi asilia Tanzania Bara, kusimamia usafirishaji au uchakataji wa mafuta ghafi au gesi asilia na kusimamia usafirishaji, kusambaza na kuuza mafuta na gesi asilia nchini.

EWURA pia ndio yenye dhima ya utoaji leseni za uendeshaji wa huduma za nishati na maji, kufanya mapitio ya ushuru, ufuatiliaji wa ubora wa viwango, usalama, afya na mazingira, kukuza na kuendeleza ushindani wenye tija na kuhakikisha upatikanaji wa huduma za mafuta na maji unakuwa endelevu.

EWURA pia ina dhima ya kuandaa sera, sheria na kanuni zitakazowezesha kukua kwa sekta ya nishati na maji na kuendelea kusimamia utoaji wa huduma bora nchini.

## KUDHIBITI UCHAKACHUAJI

Mwaka 2007 kabla ya EWURA kuanza kuvalia njuga tatizo la uchakachuaji, hasa tabia ya wafanyabiashara wasio waaminifu kuchanganya mafuta ya dizeli na ya taa ili kupata faida kubwa, uchakachuaji ulikuwa asilimia 80! Lakini sasa hivi ni chini ya asilimia tano.

EWURA ilipata mafanikio hayo baada ya kuanzisha programu ya kuweka vinasaba kwenye mafuta yanayotumika nchini. Hatua hiyo inaelezwa kwamba si tu ilisaidia kudhibiti uchakachuaji na hivyo kuweka mazingira sawia ya ushindani lakini pia kudhibiti ukwepaji wa kodi.

Tatizo la uchakachuaji, mbali na kuharibu ushindani katika biashara na kukwepa kodi, mafuta yaliyochakachuliwa husababisha mfumo wa mafuta wa magari kuharibika.

## UTUNZAJI HATARISHI WA MAFUTA

Moja ya mambo ambayo EWURA imefanya kwa mafanikio ni kuweka mfumo bora unaoondoa utunzaji na uuzaji wa mafuta katika mapipa, madumu na chupa za plastiki.

Hatua hii, mbali na kudhibiti ubora wa mafuta, imesaidia kudhibiti athari zinazoweza kutokea kwa sababu mafuta ni bidhaa inayolipika.

## BEI KIKOMO

Taarifa zilizopo zinaonesha kwamba mwezi Januari mwaka 2009, bei ya mafuta ilipanda kiholela ikiwemo kupandishwa mara tatu kwa siku.

Ni kutokana na hali hiyo mamlaka iliingilia kati na kuamua kuja na bei kikomo au elekezi. Kwa mfano, katika kipindi hicho (Januari 2009), taarifa zilizopo zinaonesha kwamba bei za mkoa wa Dar es Salaam zilishuka kutoka Sh. 2,000 hadi Sh. 1,233 kwa lita sawa na punguzo la asilimia 62.

Bei elekezi hupangwa kwa kuzingatia gharama za uagizaji, gharama za bandari na taasisi nyingine, kodi za serikali, gharama za usambazaji na pia huangalia faida anayobaki nayo mfanyabiashara.

Baada ya kupanga bei EWURA hufanya ukaguzi wa kushtukiza kwenye vituo vya mafuta ili kuona kama mafuta yanauzwa kwa bei kikomo.

## UTOAJI WA LESENI

Mbali na kuhamasisha wafanyabiashara kujenga vituo zaidi vya mafuta, EWURA inatoa leseni ili kuhakikisha huduma za mafuta zinazotolewa zinafuata sheria, kanuni na viwango stahiki.

Leseni hizi zinahusisha kuuza mafuta kwa jumla, vituo vya mafuta vya rejareja, kuhifadhi mafuta, biashara za vilainishi na kuagiza na kuuza gesi ya kupikia (LPG).

Pia kuna leseni zinazoruhusu mtu kutoa huduma ya mafuta kwenye meli, kujenga miundombinu binafsi ya kuhifadhia mafuta (consumer installation), kusafirisha mafuta, kuchakata mafuta machafu (waste oil recycling), leseni ya kusafirisha mafuta na leseni ya uwakala wa uagizaji mafuta kwa pamoja (PBPA).

## UTOAJI ELIMU

EWURA pia imekuwa ikitoa elimu kwa wafanyabiashara na wananchi kuhusu masuala mbalimbali. Kwa mfano, kufuatia majanga ya moto kama lile lilojiri Morogoro Agosti 10, 2019 na kusababisha zaidi ya watu 70 kupoteza Maisha EWURA ilianza kutioa elimu kwa jamii kujitenga na matukio hatari kama hayo.

Elimu iliyokuwa inatolewa ni pamoja na wananchi kuepuka kukimbilia maeneo ya ajali za malori au visima vya mafuta vinapolipuka ili kudhibiti matukio ya vifo vya watu na uharibifu mali utokanao na moto.

Hata wakati wa mashindano ya Kombe la Dunia yaliyokuwa yanafanyika nchini Qatar Ewura ilikuwa inatoa tangazo la elimu kwa umma kuhusu ajali ya moto utokanao na malori ya mafuta ikitaka wasikimbilie eneo la ajali bali watoe taarifa.

Kwa mujibu wa tovuti ya Ewura, kuna visima vya mafuta zaidi ya 2,500 nchini na maghala makubwa na madogo ya hifadhi za mafuta Dar es Salaam na mikoani. Mbali na bomba la mafuta la Tazama (Tanzania na Zambia), nishati hiyo husafirishwa kwa malori kutoka bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara kwenda mikoani na nchi jirani za Congo DR, Zambia, Malawi, Burundi, Rwanda, Uganda.

## MIFUMO YA KIELEKTRONIKI

EWURA imeeleza kuendelea kuboresha mifumo yake ya kieletroniki ili kuimarisha upokeaji wa taarifa za shughuli za uagizaji, uhifadhi, usambazaji na uuzaji wa nishati ya mafuta.

Hayo yameelezwa karibuni na Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Dk James Andilie, alipofanya kikao kazi na watumishi wa mamlaka hiyo Kanda ya Ziwa, jijini Mwanza.

Anasema lengo la maboresho hayo ni kuleta ufanisi zaidi katika udhibiti wa sekta ya mafuta na kukidhi kwa ufasaha dhima ya Serikali ya huduma mtandao (e-services).

Jarida hili haliuzwi

*Leo yetu ndiyo kesho yetu*

Uelekeo

JARIDA

# Jungu kuu

| Jumamosi Desemba 9 -12, 2023 |






# CCM na awamu sita za demokrasia imara

UK. 12, 13 & 16

# Rais Samia anavyopaisha elimu miaka 62 ya Uhuru

**Na Hellen Mwango**

KUTOKANA na umuhimu wake, kuna kaulimbiu nyingi kuhusu elimu kama vile; elimu ni ufunguo wa maisha, elimu ni bahari haina mwanzo wala mwisho, ukidhani elimu haina maana jaribu ujinga na nyingine nyingi.

Tanzania inaadhimisha miaka 62 tangu ipate Uhuru wake ikiwa na Rais wa kwanza mwanamke, Dk. Samia Suluhu Hassan ambaye kila mwenye macho ameona namna anavyopaisha elimu tangu ashike madaraka takribani miaka mitatu iliyopita.

## FEDHA ZA UVIKO-19

Katika kuweka kipaumbele katika elimu, Rais Samia aliamua sehemu ya fedha za mkopo kutoka Shirika la Fedha Duniani za Uviko -19 kuzielekeza kwenye miradi ya Elimu ikiwamo ujenzi wa vyumba vya madarasa shule za msingi, sekondari na katika vyuo 17 nchini.

Uamuzi wa Rais kuelekeza fedha hizo kwenye miradi mbalimbali ikiwamo kuboresha miundombinu ya shule za za msingi na sekondari ulisababisha wanafunzi wote walioandikishwa kuanza darasa la kwanza, waliofaulu kujiunga na kidato cha kwanza wote nchi nzima kuanza masomo bila kukumbana na changamoto ya uhaba wa madarasa.

Hatua hii iliongeza juhudi kwa wananchi kuchapa kazi kumuunga mkono rais katika kuhakikisha watoto wote wenye umri wa kuanza shule wanakwenda shule kujenga taifa la wasomi zaidi.

Ujenzi wa miradi hiyo pia ulitunisha mifuko ya Watanzania kwa kupata ajira za muda huku wakandarasi, wengi wakiwa wazawa wakunufaika pia kwa malipo.

## ELIMU BURE

Wakati akiingia madarakani, serikali ameondoa ada kwa wanafunzi wa chekechea hadi kidato cha nne, ili kuwapunguzia wazazi mzigo na kuhakikisha haiwi sababu ya mwanafunzi kushindwa kwenda shule.

Lakini kwa kutambua kwamba bado wazazi wenye kipato cha chini walikuwa wanashindwa kuwapeleka watoto wao kidato cha tano na cha sita, akaamua kuondoa pia ada kwa ngazi hiyo.

Hatua hiyo imeongeza idadi ya wanafunzi waliotoka kwenye familia masikini waliokuwa wanashindwa kuendelea na elimu ya kidato cha sita kutokana na ada pamoja na michango mingine ya shule.

## SAMIA SCHOLARSHIP

Samia pia amekuja na programu ya ufadhili wa wanagfunzi iitwayo Samia Scholarship kwa masomo ya shahada ya kwanza kwa wanafunzi wanaopata ufaulu wa juu katika mitihani ya Kidato cha Sita katika tahasusi za Sayansi (PCB, PCM, PGM, CBG, CBA, PMC na CBN).

Samia Scholarship inagharamia kwa asilimia mia moja masomo ya Elimu ya Juu kwa wanafunzi hao wakipata udahili katika fani za Teknolojia, Uhandisi, Hisabati na Tiba.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Adolf Mkenda hivi karibuni alisema mpango huo wa Samia Scholarship umeleta mwamko na ushindani mkubwa kwa watoto wa kike kuvutiwa kusoma masomo hayo.

## MABORESHO YA MITAALA YA ELIMU

Baada ya miaka mingi, Serikali ya Awamu ya Sita imeamua kufanya maboresho kwenye baadhi ya maeneo katika Sera ya Elimu na Mafunzo ili kutoa elimu ya ujuzi badala ya elimu ya taaluma pekee ambapo elimu ya lazima itakuwa ya miaka 10 badala ya saba kama ilivyo sasa.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa anasema utekelezaji wa maboresho hayo utaanza mwaka 2027 sambamba na kufuta mtihani wa darasa la saba na badala yake kuanza kufanyika kwa tathmini darasa la sita kwa ajili ya kujiunga na elimu ya lazima ya sekondari.

Waziri Mkuu alitoa rasmi taarifa ya serikali Novemba 2, mwaka huu kuhusu kuidhinishwa kwa Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Toleo la 2023 na Mitaala ya Elimu Ngazi ya Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Elimu ya Ualimu.

Anaelezea hatua hiyo ilifikiwa baada ya kubainika kuwepo kwa changamoto mbalimbali zikiwemo za mfumo wa elimu kujikita zaidi kwenye elimu ya jumla na kukosa fursa za elimu na mafunzo kwa kuzingatia mahitaji na njia mbalimbali za ujifunzaji kutokidhi haja kulingana na mazingira.

"Mitaala haikidhi mahitaji ya mabadiliko ya kiuchumi, kijamii, kisayansi na kiteknolojia, mfumo usio fanisi wa udhibiti na ithibati ya elimu na upungufu wa nguvu kazi. Changamoto hizo zilizaa hitaji la kuboresha sera yetu ya elimu ili kukidhi mahitaji ya sasa na wakati ujao," anasema Waziri Mkuu.

Akifafanua kuhusu maeneo yaliyoboreshwa kwenye sera hiyo anasema; "Sera ya Elimu na Mafunzo ilifanyiwa mabadiliko kwenye maeneo kadhaa ikilinganishwa na sera iliyopita kwa kuongeza fursa za elimu ya amali (elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi) ambayo itaanza kutolewa kuanzia kidato cha kwanza."

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa, Adolf Mkenda, anafafanua zaidi kwamba kuanzia mwakani (2024) elimu ya msingi itakuwa miaka sita na sekondari miaka minne, ili kuwapa fursa wanafunzi kuchagua aina ya masomo yanayopenda, kusaidia waweze kujiajiri wamalizapo masomo.

Anasema mabadiliko hayo yataenda sambamba na kufundisha lugha ya Kingereza, ambayo itaanza kufundishwa kuanzia darasa la kwanza na baada ya darasa la sita kutakuwa na mkondo wa mafunzo ya u na ufundi stadi utakaojulikana kama elimu ya amali na elimu ya jumla.

Kila mkondo kutakuwa na michepuo yake, ili kuwapa nafasi wanafunzi kuchagua masomo wanayoyataka kwa ajili ya kuendeleza ujuzi na nadharia zaidi ili wakimaliza shule waweze kuajirika au kujiajiri wenyewe.

"Kuanzia mwakani watoto watasoma hadi darasa la sita na watafundishwa lugha ya Kingereza na Kiswahili na masomo mengineyo, lakini pia kutokana na mitaala kubadilika watoto wataweza kuonesha umahiri wao katika masomo yao," anaeleza Profesa Mkenda.





Hamisi Kibari

## TUKUBALIANE KUTOKUBALIANA

Simu: 0758143457

# Tumuunge mkono Samia uhuru wa uchumi

LEO Watanzania wanaadhimisha miaka 62 ya uhuru wa Tanzania Bara (wakati huo Tanganyika) baada ya harakati zilizofanywa na waasisi wa taifa letu chini ya chama kilichomng'oa mkoloni cha Tanganyika African National Union (TANU).

Kimsingi, harakati za muda mrefu za kudai uhuru zilizaa matunda Machi 1961, wakati Mkutano wa Katiba (Constitutional Conference) ulipofanyika mjini Dar es Salaam, badala ya London.

Hii ilikuwa ni tofauti na ilivyokuwa imezoeleka kwa nchi zote zilizokuwa makoloni ya Uingereza kwa kuwa safari mazungumzo kuhusu programu ya uhuru kamili wa Tanzania Bara yalifanyika ndani ya eneo husika.

Ni kutokana na mazungumzo hayo, miezi miwili tu baadaye, yaani Mei 1, 1961, Tanganyika iliweza kupata Serikali yake yenye madaraka ya ndani, ikiongozwa na Baraza la Mawaziri 11, chini ya Mwalimu Julius Nyerere, kama Waziri Mkuu.

Pamoja na kupata madaraka, siku kubwa iliyosubiriwa kwa hamu na shauku kubwa kuliko zote zilizotangulia ilikuja Desemba 9, 1961 (usiku wa kuamkia siku kama ya leo), pale bendera ya Mwingereza, maarufu kama "Union Jack", iliposhushwa usiku wa manane; na bendera ya Tanganyika huru ikapandishwa kuchukua nafasi yake, kuashiria 'uhuru kamili' wa Tanganyika.

Katika salamu zake za uhuru, Mwalimu Nyerere alizungumzia uhuru wa kisiasa tulikuwa tumeupata akisema: "Tunasherehekea ushindi. Lakini tukumbuke kwamba ushindi tuliopata ni ile haki ya kufanya kazi wenyewe, haki ya kupanga na kujenga nchi yetu kwa uhuru, bila kuingiliwa."

Mwalimu alizungumzia pia imani ya Tanu (baadaye CCM) juu ya usawa wa binadamu na heshima kwa wote ambapo alisema: "Tumekubaliana kwamba taifa letu litakuwa la raia huru walio sawa, ambalo kila mmoja atapata fursa kutumia uwezo wake kuendeleza jamii... Hakuna kitu kitakachomwondolea haki ya kazi zake kama mjumbe wa jamii. Na hili lazima tuanze kulitekeleza." (Nyerere: Freedom and Unity, uk. 138 – 139).

Leo tunaposherehekea miaka 62 tangu nchi yetu ijiondoe kwenye minyororo ya ukoloni, ni muhimu kila Mtanzania ajiulize maswali kadhaa, mintarafu suala zima la uhuru wa uchumi.

Katika eneo la uchumi serikali yetu, hususani awamu hii ya sita inatujengea mazingira wezeshi mengi mazuri.

Kwa uchache, serikali yetu inaendelea kuboresha miundombinu ya usafiri kuanzia wa anga (uboreshaji wa shirika la ndege), barabara, reli (ujenzi wa reli ya kisasa) na wa usafiri majini (mkataba na DP World kuboresha huduma bandarini maradufu).

Serikali inapambana tupate umeme wa uhakika (Bwawa la kuzalisha umeme la Nyerere) na kusambaza umeme vijijini huku kwenye kilimo serikali imekuja na miradi ya kuboresha skimu za umwagiliaji na ile inayoshirikisha vijana ya jenga kesho yao leo (BBT) na kadhalika.

Serikali hii pia inaboresha vyema eneo la diplomasia ya uchumi ikilenga kuvutia wawekezaji wengi kuja nchini na kutafuta masoko ya bidhaa zetu.

Lingine muhimu sana kwa kumazingira wezeshi ya ukuaji wa uchumi ni nchi yetu kuendelea kuwa na amani. Tukumbuke bila amani hakuna kinachoweza kufanyika. Huwezi kuvutia wawekezaji, huwezi kufanya uzalishaji hata kwenda tu kwenye nyumba za ibada kama nchi haina amani.

Je, kila mmoja wetu kwa nafasi yake anatumia uwezo wake kuendeleza jamii kwa fursa anayopata? Je, tunamuunga vipi mkono Rais Dk. Samia ambaye amedhamiria kwa dhati kuona nchi yetu inajitegemea iuchumi na wananchi wanaondokana na umaskini?

Yapo madai kwamba kudumaa kwa uchumi wetu kwa kiasi fulani kunatokana na mbinyo wa ubeberu wa dunia ambao unaelezwa kwamba umekuwa ukihakikisha unatunyonya kadri unavyoweza kupitia taasisi zake 'mumiani' mbalimbali kama Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), Benki ya Dunia (WB), Shirika la Biashara la Kimataifa (WTO) na kadhalika.

Kuna ukweli kiasi lakini pamoja na madai hayo baadhi ya mambo yamekuwa yakisababishwa na mipango yetu mibovu, uzembe na ubinafsi wetu wa kuangalia mimi nitapata nini badala ya nchi yangu (ubadhirifu na ufisadi).

Profesa wa uchumi Mtanzania, Kitojo Wetengere alipata kuandika makala yake akisema kwamba serikali za awamu zilizopita zilifanya mambo mengi mazuri na makubwa na mengine yanayofanywa sasa ni mwendelezo wa msingi uliowekwa kwenyeawamu zilizopita.

Lakini akaonya serikali isiruhusu 'uholela' ambao wakati fulani ulisababisha nchi yetu kugubikwa na vitendo vya rushwa na ufisadi kwa sababu baadhi yetu ni wachoyo na wabinafsi.

Alihoji unawezaje, kwa mfano, kujenga uhuru wa uchumi kama mapato ya serikali yanavujia kwenye mifuko ya wachache?

Tangu serikali ya Awamu ya Tano na hii ya Sita ziingie madarakani, kumekuwa na udhibiti mzuri wa mapato ya serikali.

Tukumbuke Rais Dk. Samia Suluhu Hassan alikuwa Makamu wa Rais katika awamu iliyopita na ameendeleza yaleyale huku akiboresha hapa na pale na pengine kilichobadilika na kutotumia ukali katika kuchukua hatua isipokuwa matumizi ya kalamu.



> Viongozi, wataalamu wetu wanapaswa kutusaidia kwa haraka katika kufikia uhuru wa kiuchumi ikiwa ni pamoja na kuhakikisha hatuendelei kuuza nje mazao ghafi

Kila mwenye dhima katika ofisi ya umma, anapaswa kumuunga mkono Samia kwa kuchapa kazi, kuacha ubadhirifu wa raslimali na kujitenga na vitendo vya rushwa.

Miaka ya nyuma, kulipotokea kashfa ya usafirishaji magogo kwa wanaokumbuka, ilielezwa kwenye moja ya vyombo vya habari kwamba wizi wa raslimali uliokuwa ukifanyika katika sekta ya maliasili na utalii pekee (kwa mfano), ulikuwa maradufu ya misaada kutoka nje na mikopo iliyokuwa inaelekezwa katika kuendeleza sekta hiyo!

Hatuwezi kufikia kwenye uhuru wa uchumi kulinganisha na nchi zilizoendelea kama ofisi za umma na hata za binafsi hakuna uadilifu na uwajibikaji.

Viongozi, wataalamu wetu wanapaswa kutusaidia kwa haraka katika kufikia uhuru wa kiuchumi ikiwa ni pamoja na kuhakikisha hatuendelei kuuza nje mazao ghafi ambayo mengine yakishaongezewa thamani, tunayanunua tena nchini kwa bei maradufu!

Kwamba hatuwezi kuendelea kuagiza vifaa tiba hata vile ambavyo mali ghafi zake kama gozi na bandeji (pamba) au dripu (maji) zinapatikana nchini.

Katika muktadha wa kubinywa na ubeberu, kama tunaingia mikataba mibovu kwa hadaa na kutotilia maanani mikataba isiyo na tija, hapo machawi wetu kiuchumi anakuwa nani? Bila shaka ni sisi wenyewe.

Kimsingi serikali ya awamu ya sita, imeonekana kuyatafakari haya na mengine mengi ambayo hayajatajwa kwenye makala haya na kuona ipo haja ya kubadili mwelekeo.

Serikali imeonesha dhamira ya kweli ya kutupeleka kwenye uhuru wa kiuchumi ikija na mikakati ya kuboresha kilimo cha kisasa na kuhimiza ujenzi wa viwanda, hivyo na tunapaswa kuishukuru na kuiunga mkono.

Kama wananchi tutaiunga mkono kwa dhati serikali hii na kuchapa kazi kwa bidii, muda si mrefu Tanzania nayo itaanza kutoa misaada kwa nchi zingine kama nchi mfadhili kama alivyokuwa anatamani kuona Rais wa Awamu ya Tano.

MIAKA 62 YA UHURU

# CCM na awamu sita za dem

**Na Hamid Yassin**

LEO, Tanzania Bara inatimiza miaka 62 ya Uhuru huku ikiwa na mambo mengi mazuri ya kujivunia.

Kubwa likiwa ni kuendeleza msingi wake mkubwa wa amani, utulivu, umoja na demokrasia thabiti chini ya Awamu Sita za Serikali madhubuti ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Ndani ya miaka hii 62 ya Uhuru zipo changamoto kadhaa za hapa na pale, lakini zinafunikwa na mambo mengi mazuri yaliyosheheni pande zote za Tanzania. Moja ya hayo ni mfumo wa kidemokrasia unaolenga kubadilishana madaraka kupitia chaguzi mbalimbali.

Kupitia machapisho na kumbukumbu mbalimbali asilimia kubwa ya Watanzania wanaelewa jinsi Uhuru wa Tanganyika (Tanzania Bara baada ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar) ulivyopatikana; hivyo makala haya hayataongelea sana hilo bali yanajikita kwenye baadhi ya masuala mbalimbali yanayojiri baada ya uhuru huo.

**MWALIMU NYERERE**

Huwezi kuzungumzia Uhuru wa Tanganyika bila kumtaja Baba wa Taifa hili, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Huyu alikuwa binadamu maalumu si Tanzania tu, bali Afrika! Kwani akiwa ana miaka 39 tu aliiwezesha Tanganyika kupata uhuru na alifanikiwa kuifanya Tanganyika kuwa Jamhuri na yeye kuwa Rais wa kwanza akiwa na miaka 40 tu!

Mwalimu hakuchelewa, mara baada ya uhuru akatafakari jinsi ya kuiondoa Tanganyika kwenye ile taswira ya kikoloni na kuwa taifa lenye mtazamo wake wa kusaka maendeleo na jinsi ya kuwakwamua raia wake kwenye mazonge ya wakoloni!

Aliibuka na masuala kadhaa, huku kubwa likiwa kutambulisha siasa ya ujamaa na kujitegemea.

Ujamaa ni neno la Kiswahili linalomaanisha familia, jamii moja au neno linalokaribia hilo ni 'undugu'.

Kinyume na ubepari, ujamaa ni mfumo uliolenga Watanzania kuishi katika misingi ya usawa, utu, umoja na huku ukijitenga na kundi moja la Watanzania kuwanyonya Watanzania wenzao kiuchumi.

Ni mfumo ambao ulilenga kuweka njia kuu za uchumi mikononi mwa umma na si kundi la watu wachache.

Nyerere alitafsiri dhana ya Ujamaa kuwa mfumo wa usimamizi wa kisiasa na wa kiuchumi kwa namna mbalimbali.

Mosi, alitaka kuweko kwa mfumo wa chama kimoja chenye uongozi madhubuti ambacho kwa wakati ule kilikuwa ni Tanganyika African National Union (TANU) ili kusaidia katika kuimarisha mshikamano wa kujitegemea kwa Tanganyika iliyokuwa imetoka kujipatia uhuru.

Mbili, ustawishaji wa usawa kijamii, kiuchumi na kisiasa kwa kuweko kwa demokrasia, kukomesha ubaguzi kwa misingi ya hali ya mtu na kufanya matunda ya sekta muhimu za uchumi kuwafikia watu wote.

Tatu, pia alitaka kupeleka uzalishaji katika vijiji na hivyo kuunda vijiji vya ujamaa ili kuwezesha wananchi kupata huduma za kijamii na kiuchumi kwa urahisi huku wakiwa na uwezo wa kufanya uzalishaji kwa pamoja.

Nne, kukuza dhana ya kujitegemea kwa Tanganyika kwa njia mbili; mabadiliko ya kiuchumi na mitazamo ya kiutamaduni. Kiuchumi, kila mtu angekifanyia kikundi chote kazi na kujifanyia yeye mwenyewe; kiutamaduni, ilikuwa ni lazima Watanganyika wajifunze kujikomboa kutoka utegemezi wa nchi za Ulaya.

Tano, Mwalimu Nyerere alipanga utekelezaji wa elimu bila malipo na ya lazima kwa wote.

**MUUNGANO TANGANYIKA NA Z'BAR**

Ndani ya miaka mitatu tu ya uhuru, chini ya uongozi wa Mwalimu Nyerere, Tanganyika iliungana na Zanzibar na kuzaliwa taifa la Tanzania.

Mkataba huo wa Muungano ulitiwa saini na aliyekuwa Rais wa Tanganyika, Hayati Mwl. Julius Nyerere na aliyekuwa Rais wa Zanzibar, Hayati Abeid Amani Karume, Aprili 22, 1964 huko Zanzibar.

Ulithibitishwa na Bunge la Tanganyika na Baraza la Mapinduzi hapo Aprili 26, 1964 na ilipofika Aprili 27, mwaka huo huo, viongozi wa nchi zote mbili walikutana katika Ukumbi wa Karimjee jijini Dar es Salaam na kubadilishana Hati za Muungano.

Sheria za Muungano wakati ule zilitoa tamko la Jamhuri katika Ibara ya 4 ikiwa na maana; Jamhuri ya Watu wa Zanzibar italazimika siku zote baada ya kuungana, kuunganishwa kuwa Dola ya Jamhuri kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar (Ibara ya 4 Sheria za Muungano).

Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar lilibadilishwa baadaye Oktoba 28, 1964 na kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kupitisha Sheria ya Jamhuri ya Muungano, Sheria namba 61 ya mwaka 1964.

Uongozi wa Mwalimu Nyerere uliijengea Tanzania heshima ya kimataifa kutokana na msisitizo wake wa maadili kama msingi wa maamuzi ya siasa.

Chini ya Nyerere Tanzania ilipiga hatua kubwa katika vipengele mbalimbali vya maendeleo; vifo vya watoto vilipungua kutoka watoto138 kati ya 1,000 waliozaliwa hai mwaka 1965 hadi watoto110 mwaka 1985; tarajio la kuishi lilipanda kutoka miaka 37 (1960) hadi miaka 52 (1984).

Uandikishaji wa wanafunzi katika



shule ya msingi ulipanda kutoka asilimia 25 (huku watoto wa kike ilikuwa asilimia 16) mwaka 1960 hadi asilimia 72 (watoto wa kike nao ikiongezeka hadi asilimia 85) mwaka 1985.

Ingawa idadi ya wananchi ilikuwa inaongezeka kwa kasi, asilimia ya watu wazima waliojua kusoma na kuandika ilipanda kutoka asilimia 17 mwaka 1960 hadi asilimia 63 mwaka 1975. Hii ilikuwa juu sana kuliko nchi nyingine za Afrika.

Hata hivyo, ujamaa ulishindwa kuibeba Tanzania kiuchumi kufuatia matatizo mbalimbali yaliyoikumba nchini kama vile upungufu mkubwa wa mafuta miaka ya 1970, anguko la bei ya bidhaa zilizozalishwa nchini (hasa kahawa na katani), utovu wa uwekezaji kutoka nje ya nchi na vita vya Uganda na Tanzania mwaka 1978 hadi 1979 vilivyotumia rasilimali nyingi na miaka miwili mfululizo ya ukame.

Kufikia mwaka 1985 ilikuwa wazi kwamba ujamaa ulishindwa kuitoa Tanzania kwenye ufukara na ni katika kipindi hicho Mwalimu Nyerere alitangaza kung'atuka madarakani.

Baada ya Mwalimu nchi iliongozwa na Rais Ali Hassan Mwinyi aliyeingiza nchi katika uchumi wa soko huria.

**AZIMIO LA ARUSHA**

Azimio la Arusha ni tamko rasmi la kisiasa lililokusudia kuilekeza Tanzania katika kujenga Ujamaa. Jina hilo lilitokana na kikao kilichofanyika mjini kati ya Januari 26 hadi 29 mwaka 1967.

Tarehe 5 Februari mwaka 1967 Mwalimu Nyerere alilitangaza hapa Dar es Salaam kama uamuzi wa Watanzania wa kuondoa unyonge wao.

Tamko lile la Arusha lilikuwa lina sehemu tano; Itikadi ya chama cha TANU, siasa ya ujamaa na kujitegemea, uanachama wa TANU na Azimio la Arusha.

Kiini chake kilikuwa ni hiki; "Tulionewa kiasi cha kutosha, tulinyonywa kiasi cha kutosha, tulipuuzwa kiasi cha kutosha. Unyonge wetu ndio uliotufanya tuonewe, tunyonywe na kupuuzwa.



Sasa tulitaka mapinduzi, mapinduzi ya kuondoa unyonge ili tusionewe tena, tusinyonywe tena na tusipuuzwe tena".

**ALI HASSAN MWINYI**

Mzee Ali Hassan Mwinyi aliyezaliwa Mei 8 mwaka 1925 alikuwa Rais wa pili wa Tanzania kuanzia mwaka 1985 hadi 1995. Kama tulivyokwishaona, mtangulizi wake katika kuongoza nchi yetu alikuwa Mwalimu Nyerere, na aliyemfuata ni Benjamin Mkapa. Pia alikuwa Mwenyekiti wa CCM Taifa kuanzia mwaka 1990 hadi 1996.

Kabla ya hapo alikuwa Rais wa tatu wa Zanzibar baada ya kujiuzulu kwa mtangulizi wake, Aboud Jumbe Mwinyi Januari 1984. Urais wa Zanzibar ulimfanya kuwa Makamu wa Rais wa Tanzania; hivyo aliteuliwa kugombea urais wa kitaifa wakati Julius Nyerere alipoamua kutogombea tena mwaka 1985.

Mwinyi alichaguliwa, akaacha cheo chake cha urais wa Zanzibar, akawa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nafasi ya kuongoza Zanzibar ilizibwa na Idris Abdul Wakil.

Wakati wa urais wa kitaifa wa Mwinyi, ndipo sera za ujamaa zilianza kugeuzwa taratibu ili kwenda na hali halisi ya wakati huo kwa maana ya kukaribisha uliberari katika uchumi. Masharti ya kuingiza bidhaa kutoka nchi za nje yalipunguzwa na uanzishaji wa biashara ya watu binafsi ulihamasishwa.

Hatimaye mzunguko wa fedha ulikuwa mkubwa hapa nchini, Watanzania wakafurahi sana kiasi cha kumpachika jina la utani kiongozi huyo la 'Mzee Ruksa'!

Mwaka 1991, Rais Mwinyi alianzisha Tume ya Nyalali iliyopendekeza kuanzisha mfumo wa vyama vingi nchini. Wakati akimaliza awamu yake ya pili ya uongozi mwaka 1995 nchi iliendesha uchaguzi wa kwanza wa

MIAKA 62 YA UHURU

# okrasia imara





vyama vingi vya kisiasa.

Mwinyi, baada ya kustaafu, hakujiingiza katika mambo ya siasa ya kila siku. Anaendelea kuishi hapa Dar es Salaam kwa raha mustarehe!

**BENJAMIN MKAPA**

Benjamin William Mkapa aliyezaliwa Novemba 12, mwaka 1938, huko Lupaso, Wilaya ya Masasi, alikuwa Rais wa awamu ya tatu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kati ya mwaka 1995 na 2005. Pia alishika wadhifa wa Uwenyekiti wa CCM Taifa.

Wakati wa kampeni za kwanza baada ya mfumo wa vyama vingi kurejeshwa nchini mwetu mwaka 1995, msingi wa kampeni za Mkapa ulikuwa ni kupambana na ufisadi na alikuwa akiungwa mkono kwa nguvu na Rais wa Awamu ya Kwanza, Mwalimu Nyerere. Ikumbukwe pia Mkapa alikuwa mwanafunzi wa Mwalimu Nyerere wakati akifundisha Sekondari ya Pugu.

Juhudi za Mkapa za kupambana na ufisadi alipoingia madarakani ni pamoja na kuunda jukwaa la wazi lililoitwa Tume ya Rais ya Ufisadi (Tume ya Warioba) na kuongeza msaada kwa ofisi za kupambana na ufisadi ikiwemo Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru). Tume ya Warioba pia ilisaidia katika kutambua vyanzo vya rushwa nchini na namna ya kupambana navyo.

Akiwa ofisini, Mkapa ambaye sasa ni marehemu, alibinafsisha kampuni zilizomilikiwa na serikali sambamba na kuendeleza sera za soko huria za Mzee Mwinyi. Pamoja na maneno ya hapa na pale kutoka kwa wanasiasa wa kambi ya upinzani, wananchi walimtetea kwa kuvutia uwekezaji wa kigeni ambao ulisaidia kukuza uchumi wa nchi.

Sera zake zilipata msaada wa Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) na kusababisha baadhi ya madeni ya nje ya Tanzania kufutiliwa mbali.

Kumbuka hayati Mkapa ndiye alikuwa rais wa kwanza baada ya kurejeshwa rasmi mfumo wa vyama vingi hapa nchini, hivyo alikutana na nyakati ngumu sana katika vipindi vyake vyote viwili, hususani, kutoka kwa viongozi wa vyama vya siasa na vya wanaharakati.

Wakati anagombea katika kipindi chake cha kwanza alikutana mwanasiasa aliyetoka kujizolea umaarufu mkubwa ndani ya CCM, marehemu Augustine Lyatonga Mrema ambaye alihamia chama kilichosheheni wasomi na wanaharakati cha NCCR-Mageuzi ambako moja kwa moja alikabidhiwa wadhifa wa uenyekiti na kupitishwa kuwa mgombea wa chama hicho.

Mkapa, maarufu 'Mzee wa Ukweli na Uwazi', katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 1995 alipata kura 4,026,422 sawa na asilimia 61.82 na kumgaragaza Mrema aliyepata kura 1,808,616 sawa na asilimia 27.77.

Katika kipindi chake cha pili na cha mwisho cha uongozi, chama cha NCCR Mageuzi kilikuwa kimepoteza mweleko kutokana na vurugu na sintofahamu za mara kwa mara ndani ya chama hicho, hususani, kati ya Mrema na Katibu wake Mkuu, Mabere Nyaucho Marando. Hali hiyo ilitoa mwanya kwa Chama cha Wananchi (CUF) chini ya uenyekiti wa Prof. Ibrahimu Lipumba na Katibu wake Mkuu, marehemu Maalim Seif Sharif Hamad kuwa chama kikuu cha upinzani.

Kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka 2000, Mkapa alifanya vizuri zaidi kuliko mwaka 1995, kwa kupata kura 5,863,201 sawa na asilimia 71.74 ya kura zote huku mpinzani wake wa karibu, Profesa Lipumba akiambulia kura 1,329,077 sawa na asilimia 16.26.

Hayati Mkapa aliinua sana uchumi wa nchi, huduma na dawa zilianza kupatikana kwenye hospitali zote za umma. Wafanyakazi wote wa serikali na sekta za umma wakaanza kuwa na uhakika wa mishahara yao kwa wakati na kusababisha ile migogoro ya kikazi, maandamano ya wafanyakazi yaliyokithiri wakati wa awamu ya pili kukoma!

Mbali ya kuzipoteza zile kampuni za 'mifukoni' za wajanja wa mjini, hayati Mkapa aliendelea kuitengeneza nchi katika kila sekta, kama vile kwenye miundombinu ambako yeye ndiye alianza kukarabati barabara na madaraja yetu sambamba na kujengea nyingine mpya chini ya Waziri wake mahiri wa Ujenzi, hayati John Pombe Magufuli.

JAKAYA MRISHO KIKWETE

Jakaya Mrisho Kikwete alikuwa Rais wa Awamu ya Nne wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tangu tarehe 21 Desemba 2005 hadi tarehe 5 Novemba 2015.

Alizaliwa Oktoba 7 mwaka 1950 katika Kijiji cha Msoga, Kata ya Lugoba, Tarafa ya Msoga, Jimbo la Uchaguzi la Chalinze, Wilaya ya Bagamoyo, mkoani Pwani. Alizaliwa katika familia ya wanasiasa. Babu yake Mzee Mrisho Kikwete alikuwa Chifu wa Wakwere. Baba yake alikuwa Mkuu wa Wilaya Pangani, Same na Tanga.

Akiwa na kaulimbiu yake ya Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya, mwaka 2005 Kikwete aliteuliwa kuwa mgombea wa CCM kwa nafasi ya rais. Akashinda uchaguzi huo wa 2005 kwa kuzoa kura 9, 123952 sawa na asilimia 80 za kura zote dhidi ya mpinzani wake aliyemfuatia, Profesa Ibrahimu Lipumba aliyepata kura 1,327,125 sawa na asilimia 11.68.

Awamu yake ya pili alipambana na mgombea wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Dk. Willibrod Slaa. Hapa chama hiki kilikuwa kimekuja juu kwelikweli baada ya kuwa msindikizaji katika chaguzi tatu za awali za mfumo wa vyama vingi.

Pamoja na nguvu za Chadema na baadhi ya washirika wake, Kikwete, akiwa ameboresha kaulimbiu yake na kuwa Nguvu zaidi, Ari zaidi na Kasi zaidi, alishinda kwa asilimia 62.83 baada ya kupata kura 5,276,827 huku Dk. Slaa akipata kura 2,271491 sawa na asilimia 27.05 ya kura zote zilizopigwa.

Katika kipindi hiki cha miaka 10 ya uongozi wa Kikwete demokrasia ilitamalaki vyema nchini. Hata ukiwauliza leo viongozi karibu wote wa vyama vya upinzani watakujibu kwamba, 'waliinjoi' kipindi kile cha rais yule wa 'maisha bora kwa kila Mtanzania!'

Mara kwa mara wapinzani walialikwa Ikulu kubadilishana mawazo na Kikwete ambako walipata mianya ya kupenyeza kero zao sambamba na kupata chakula cha pamoja na Rais.


Miaka yote 10 ya Awamu hii ya Nne ya uongozi wa nchi yetu, wapinzani waliruhusiwa kufanya siasa nyakati zote ikiwemo ile mikutano ya ndani na ya hadhara.

***Inaendelea uk. 16***

TPA
TANZANIA PORTS AUTHORITY

MIAKA 62 YA UHURU

# Rais Samia alivyodhamiria kuipeleka bandari *'next level'*




Bandari ya Dar es Salaam

> **Kwa mujibu wa takwimu kutoka Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi faida za uwezekaji zitakazofanywa na kampuni ya DP World zitaifanya Tanzania iwe pia tishio kwa washindani wake.**

**Na Hamisi Kibari**

HISTORIA ya sekta ya bandari ya Tanzania inaanzia mwaka 1893 wakati reli kati ya Tanga na Dar es Salaam ilipojengwa na kufuatiwa na ujenzi wa bandari ya Dar es Salaam mwaka 1905.

Kutoka mwaka 1947 hadi 1967, shughuli za bandari nchini zilikuwa chini ya Shirika la Reli la Afrika na Bandari la Mashariki. Kuanzia mwaka 1967 hadi 1977, jina hilo lilibadilika na kuwa Shirika la Bandari la Afrika Mashariki likiwa chini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mwaka wa 1977, Jumuiya ya Afrika Mashariki ilivunjika na Tanzania ikalazimika kuanzisha shirika lake kwa jina la Mamlaka ya Bandari ya Tanzania (THA) ili kutekeleza shughuli zilizokuwa zikifanywa na Shirika la Bandari la Afrika Mashariki.

Mwaka 2004, Bunge la Tanzania lilipitisha Sheria ya Mamlaka yaUsimamizi wa Bandari ya Tanzania nambari 17, na kuanzisha Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA). Mamlaka ilianza kufanya kazi mwaka 2006.

Moja ya vitu muhimu vilivyobadilika kutoka THA kwenda TPA ni kwamba sasa bandari zote nchini zinapaswa kisheria kuwa chini ya TPA.

Bandari ni eneo lolote la kando ya bahari, ziwa au mto ambalo chombo cha majini kitasimama kwa sababu yoyote ile hata kama ni kwa kusubiria upepo mkali upite.



Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Usimamizi Bandari Tanzania (TPA), Plasduce Mbossa

**MATUKIO MUHIMU**

Taarifa zilizopo zinaonesha kwamba ujenzi wa sehemu ya kuundia majahazi Bandari ya Dar es Salaam ulianza mwaka 1901 na baadaye ukaendelea mpaka Mwanza.

Kisha mwaka 1912 ujenzi wa bandari ya Kigoma ukaanza na kufuatiwa na ujenzi wa bandari ya Tanga mwaka 1914.

Chuo cha kusimamia shughuli za reli na huduma za bandari kilichoitwa Tanzania Railways and Port Services Institution kilianzishwa mwaka 1927 na mwaka 1954 Bandari ya Mtwara ikaanza kujengwa.

Ujenzi wa bandari za Mwanza, Bukoba, Nansio, Musoma na Itungi katika Ziwa Victoria na Ziwa Nyasa zilianza kujengwa miaka 1950 na mwaka 1953 upanuzi wa lango la bandari ya Dar es Salaam ukafanyika.

Ujenzi wa gati namba 1 mpaka 3 ulikamilika Dar es Salaam mwaka 1956 na mwaka 1958 ukawa wa ujenzi wa Kurasini Oil Jet (KOJ) ambapo mwaka 1967 ujenzi wa Kituo cha Kuhifadhia Makasha kilichopo Ubungo ulifanyika.

Mwaka 1968 ujenzi wa gati namba 4, 5 na 6 ulianza na mwaka 1969 Shirika la Bandari la Afrika Mashariki lilianzishwa baada ya kutenganisha Reli na Bandari.

Mwaka 1977 kama tulivyokwishaeleza Mamlaka ya Bandari (Tanzania Harbors Authority) ilianzishwa baada ya kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki na mwaka 1978 ujenzi wa gati namba 9, 10 na 11 katika Bandari ya Dar es Salaam ukakamilika.

Mwaka 1984 serikali ilianzishwa kwa Chuo cha Bandari kilichopo Dar es Salaam na mwaka 1988 gati namba 9, 10 na 11 zilibadilishwa na kuwa kitengo rasmi cha Makontena.

Mwaka 1989 ghala la nafaka bandari ya Dar es Salaam lilijengwa, mwaka 1998, kina cha mlango wa Bandari ya Dar es Salaam kiliongezwa kuruhusu meli kuingia bandarini mchana na usiku na kitengo cha kontena kilikabidhiwa kwa mwendeshaji binafsi (TICTS) mwaka 2000.

Mwaka 2004, Sheria iliyounda TPA ikapitishwa na Bunge kwa ajili ya kumiliki na kusimamia shughuli zote za bandari za mwambao wa Bahari, maziwa na mito.

Mwaka 2008 bandari kavu binafsi (Inland Container Depots) zilianza kutumika kuhudumia shehena ya kontena katika bandari ya DSM na mwaka 2009 mpango mkakati wa kuendeleza bandari (Ports Master Plan) 2008 – 2028 ulikamilika.

Mwaka 2010 Ukarabati wa bandari zilizo katika maziwa ulianza, na unaedelea wakati 2017 miradi ya upanuzi wa Bandari ya Dar es Salaam na uboresha wa Bandari ya Mtwara

>>> Inaendelea uk. 15

MIAKA 62 YA UHURU

# Rais Samia alivyodhamiria kuipeleka bandari *'next level'*

>>> Inatoka uk. 14

ulianza na kwa sehemu kubwa umekamilika.

**BANDARI YA DAR ES SALAAM**

Bandari ya Dar es Salaam ndio kubwa kuliko zote nchini, ikipokea au kusafirisha zaidi ya asilimia 80 ya mizigo yote.

Ni kutokana na hilo kumekuwa na maboresho mengi katika bandari hiyo ili kuimarisha huduma na hivyo kupunguza siku za mzigo kukaa bandarini sambamba na kuimarisha ulinzi na usalama wa wateja na mizigo yao.

Maboresho ya karibuni yalikuwa ni pamoja na kujenga gati lenye uwezo wa kukaa magari 10,000. Hii ilikwenda sambbamba na upanuzi wa lango la meli kuingilia na kutoka.

Kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama pia uliimarishwa ambapo sasa hauishii kwenye bandari pekee bali hata nje ya bandari ikiwa ni pamoja na kwenye bandari kavu.

Bandari imekuwa na mifumo na usimamizi mzuri wa ukaguzi na ulinzi wa mizigo inayoingia na kutoka katika katika kuhakikisha usalama wake na usalama wa walaji.

Katika kuwapunguzia usumbufu wateja, matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama) yamekuwa yakiwezesha watu kufanya malipo kwa njia ya mtandao na hata kufuatilia mizigo yao. Mengi mteja anawea kuyaona akitembelea www.ports.go.tz.

Ili kusogeza huduma katika nchi ambazo zinategemea bandari za Tanzania, TPA imefungua ofisi katika nchi hizo na hivyo kuwawezesha wafanyabiashara kutokuwa na sababu ya kusafiri hadi Dar es Salaam.

TPA imefungua ofisi katika jiji la Lusaka nchini Zambia, Kigali nchini Rwanda, Lubumbashi katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo na Bujumbura nchini Burundi. Katika maeneo mengine TPA pia ina mawakala.

Mbali na kusafirisha mizigo, wateja wanaweza kufikisha malalamiko yao katika ofisi hizi na kupatiwa ufumbuzi kwa wakati.

**BANDARI NYINGINE**

Ukiondoa Bandari ya Dar es Salaam, katika mwambao wa Bahari ya Hindi kuna bandari nyingine mbili kubwa za Mtwara na Tanga. Lakini pia ziko bandari ndogo kama za Lindi, Kilwa Masoko, Pangani, Bagamoyo, Mafia na Kwale.

Bandari zilizo chini ya TPA katika Ziwa Victoria ni Bandari ya Mwanza Kaskazini na Kusini, Nansio (Ukerewe), Kemondo Bay na Bukoba (Kagera) na Bandari ya Musoma (Mara).

Katika ziwa Tanganyika kuna bandari za Kigoma, Kasanga, Kibirizi, Kagunga, Kipili, Kabwe na Kirando.

Kwa upande wa Ziwa Nyasa bandari kubwa ni Itungi, Mbamba Bay, Liuli, Manda na Ndumbi.

**BANDARI KWENDA NEXT LEVEL**

Tanzania ni nchi inayozungukwa na nchi nyingi ambazo hazina bandari pengine kuliko nchi nyingi za Afrika wakiwemo majirani zetu ambao ni washindani wetu katika biashara ya bandari.

Nchi zinazoweza kutegemea bandari ya Dar es Salaa ni Zambia, Malawi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Burundi, Rwanda na Uganda. Lakini hata nchi zanye bandari katika baadhi ya maeneo pia zinategemea bandari za Tanzania hasa inapokuwa na ufanisi mkubwa kama Msumbuji, Kenya na hata visiwa vya Comoro

Hata hivyo, kumekuwa na ushindani mkubwa ambao unahitaji uwekezaji mkubwa sambamba na usimamizi mkubwa na wa kisasa katika shughuli za bandari na hasa kwa kuzingatia kwamba nchi yetu imekuwa ikiboresha miundombinu ya reli kwa maana ya reli ya kisasa itakayorahisisha usafirishaji wa mizigo kati ya Bandari ya Dar es Salaam kwenda bara na nchi zinazoitegemea.

Ni kwa mantiki hiyo serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan imedhamiria kukata 'mzizi wa fitina'.

Imeingia mkataba na mwekezaji, kampuni ya DP World ya Dubai, ambayo inahudumia bandari zaidi ya 160 duniani kote huku ikiwa na meli zaidi ya400. Kumbuka mpaka sasa serikali haina meli yoyote ya mizigo kwa ajili ya safari za baharini ukiacha maziwa.

Kwa mujibu wa takwimu kutoka Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi faida za uwezekaji huo zitakazoifanya Tanzania iwe pia tishio kwa washindani wake ziko lukuki. Baadhi ya hizo ni zifuatazo:-

1.Kupunguza muda wa meli kukaa nangani kutoka siku tano kwa sasa mpaka saa 24 tu.

2. Kuongeza idadi ya meli zitakazokuja Bandari ya Dar es Salaam kutoka meli 1,569 zilizohudumiwa mwaka 2021/22 hadi kufikia takriban meli 2,950 ifikapo mwaka 2032/33;

3. Kupunguza muda wa ushushaji wa makontena kutoka wastani wa siku 4.5 mpaka siku 2.

4. Kupunguza muda wa uondoshaji mizigo kutoka saa 12 mpaka saa moja tu kutokana na uboreshaji wa mifumo y Tehama.

5. Kupunguza gharama ya usafirishaji wa shehena kutoka nchi za nje kwenda nchi za jirani, kutoka USD 12,000 mpaka kati ya USD 6,000 na USD 7,000 kwa kontena.

6. Kuongezeka kwa shehena inayohudumiwa kutoka tani milioni 18.41 kwa mwaka 2021/22 hadi kufikia tani milioni 47.57 mwaka 2032/33

7. Kuongezeka kwa mapato ya serikali yatokanayo na kodi ya forodha inayokusanywa katika shehena inayopitishwa bandarini kutoka Shilingi trilioni 7.76 kwa mwaka 2021/22 hadi Shilingi trilioni 26.70 kwa mwaka 2032/33.

8. Kuongezeka kwa ajira zinazotokana na shughuli za bandari kutoka 28,990 kwa mwaka 2021/22 hadi 71,907 ifikapo mwaka 2032/33.

9. Maboresho ya magati ya kuhudumia majahazi na abiria ikiwa ni pamoja na kushawishi uingiaji wa meli kubwa za kitali (cruise ships) zitakazoongeza idadi ya watalii nchini na kuongeza pato la taifa.

10. Mafunzo ya kuwajengea uwezo wafanyakazi wa TPA katika Bandari zote.

11. Uanzishaji wa maeneo huru ya kiuchumi na kuchochea ukuaji wa sekta zingine za kiuchumi zikiwemo: sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi; utali; viwanda na biashara

12. Kuchagiza ukuaji wa sekta ndogo za usafirishaji kwa njia ya reli (SGR, TAZARA na MGR) na barabara; na kuimarisha mahusiano ya kidiplomasia.

> **Kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama pia uliimarishwa ambapo sasa hauishii kwenye bandari pekee bali hata nje ya bandari ikiwa ni pamoja na kwenye bandari kavu.**




Rais Dk. Samia Suluhu Hassan



Meli ya Umoja katika Bandari ya Mwanza Kusini

# MIAKA 62 YA UHURU



*Inatoka uk. 13*

Pia ni katika kipindi hiki ambacho Mwenyekiti wa Chama cha NCCR-Mageuzi, James Mbatia alichaguliwa kuwa Mbunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia wabunge 10 wa kuteuliwa na Rais.

Kama ilivyokuwa katika awamu za watangulizi wake, Dk. Kikwete naye aliendeleza yale mazuri na kuacha yale yaliyoonekana hayana mantiki mbele ya Watanzania.

Alizunguka dunia nzima kusaka wawekezaji na kuimarisha uhusiano wa kimataifa. Alifanikiwa sana kushawishi wawekezaji kuja nchini na kuwekeza kwenye sekta mbalimbali kama vile kwenye kilimo, viwanda, utalii, madini, uvuvi na kuongeza nguvu katika kuimarisha miundombinu.

Kikwete pia alitupia jicho kwenye sekta ya afya na elimu ambako hospitali, shule na vyuo vikuu viliboreshwa vilivyokuwepo na kujengwa vingine vipya kila kona hapa nchi.

Unapozungumzia sekondari za kata, hizo zilianza Awamu ya Nne, unapojadili mfumuko wa vyuo vikuu vingi kikiwemo kile kikubwa kuliko vyote cha Dodoma (UDOM), hiyo ni shughuli ya Mzee wa Msoga, Mrisho Jakaya Kikwete.

### DK JOHN POMBE MAGUFULI

Dk. John Pombe Magufuli alizaliwa Oktoba 29 mwaka 1959. Oktoba 29 mwaka 2015, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilimtangaza kuwa Rais wa Awamu ya Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia CCM.

Katika uchaguzi huo wa mwaka 2015, Magufuli alipata ushindi wa kura 8,882,935 sawa na asilimia 58.46 huku aliyekuwa mpinzani wake wa karibu Edward Lowassa kupitia Chadema akipata kura 6,072848 sawa na asilimia 39.97.

Sambamba na Makamu wake wa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan ambaye alikuwa ni mwanamke wa kwanza nchini kushika wadhifa huo, Dk. Magufuli aliapishwa Novemba 5, mwaka 2015, kama Rais wa tano wa Tanzania.

Ndani ya mwezi mmoja tangu alipoingia madarakani alianza kudhibiti matumizi mabaya ya fedha ndani ya serikali kwa kufuta baadhi ya sherehe zisizo na ulazima pamoja na kupambana kwa dhati na wakwepa kodi.

Hivyo alifanikiwa kujenga imani ya wananchi wengi wa Tanzania ambao kwa kiasi kikubwa walionyesha kuchoshwa na rushwa na uwajibikaji duni wa watumishi wa serikali na kada nyingine mbalimbali za sekta ya umma na binafsi.

Baada ya miaka yake mitano ya kusimamia vyema raslimali za nchi, kupambana na ufisadi na kutumbua majipu, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilimtangaza tena mshindi pamoja na makamu wake wa rais, Mama Samia kwenye uchaguzi wa Oktoba 28, mwaka 2020.

Katika uchaguzi huo, Magufuli alipata kura 12,516,252 sawa na asilimia 84.4 dhidi ya mgombea kinara wa kambi ya upinzani, Tundu Lissu aliyeambulia kura 1,933271 sawa na asilimia 13.04.

Rais Magufuli alisifika kwa ufanyaji kazi hodari kama mtu asiyekubali umaskini unaosababishwa na watu, hasa kwa wafanyakazi wake. Pia alikuwa mtu anayependa haki sawa kwa wote na kuchukia rushwa, ambayo alifaulu kuipunguza kwa kiasi fulani, pamoja na kutambua na kuondoa wafanyakazi hewa na watumishi wasio na sifa serikalini.

Pia alipinga kwa vitendo dhuluma ya kiuchumi kutoka kwa kampuni zinazochimba madini mbalimbali nchini kwa kunufaika zenyewe huku nchi ikibaki na hasara.

Ni katika muktadha huo, kampuni kama Barrick ilikubaliana na serikali kufuta kampuni tanzu ya Acacia na kuanzisha mpya ya Twiga ambamo serikali inamiliki asilimia 16 za hisa hivi sasa.

Pia alifanikisha azimio la miaka mingi la serikali kuhamia Dodoma. Kwani yeye mwenyewe alihamia huko Oktoba, mwaka 2019; Jiji lililoteuliwa tangu enzi ya Awamu ya Kwanza ya Mwalimu Nyerere kuwa makao makuu ya nchi.

Hata hivyo, baadhi wapingaji wake (critics) waliona kama anafinya uhuru wa vyama vya upinzani na uhuru wa vyombo vya habari. Lawama hizo ziliigharimu Tanzania kunyimwa misaada mbalimbali.

Rais Magufuli, akiwa bado madarakani, alifariki dunia Machi 17, mwaka 2021 katika hospitali ya Mzena ya jijini Dar es Salaam alikokuwa anatibiwa. Makamu wa Rais, Samia ndiye alitangaza msiba huo mkubwa na kisha akatangaza kipindi cha siku 14 cha maombolezo ya kitaifa.

### SAMIA SULUHU HASSAN

Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Samia Suluhu Hassan, alizaliwa Januari 27, mwaka 1960.

Kabla ya kuwa rais kutokana na kifo cha John Magufuli, kilichotokea 17 Machi, 2021, Samia alikuwa Makamu wa Rais kwa sababu ya kuwa mgombea mwenza kuanzia uchaguzi mkuu wa 2015 na kisha uchaguzi wa mwaka 2020.

Ni rais wa kwanza mwanamke na wa pili kutoka Zanzibar, baada ya Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Awamu ya Pili.

Baadhi ya watu walidhani asingeweza kuvaa viatu vya Magufuli vikamtosha au angepuuza mambo kadhaa ya mtangulizi wake huyo. La hasha! Ameendeleza yote mazuri ambayo pia alishiriki kuyajenga alipokuwa Makamu wa Rais; na kama kawaida, yale yote ambayo ameona hayafai kuendelezwa ameyaweka kando 'kistaarabu sana'!

### KUBORESHA DEMOKRASIA

Tangu aingie madarakani Machi 19, 2021, Rais Dk. Samia amekuwa akijipambanua kama kiongozi anayeongoza kwa kutumia nguzo nne ambazo zinalenga katika kuliunganisha Taifa la Tanzania katika nyanja zote zikiwemo za kisiasa, kijamii, kiuchumi na kiutamaduni.

Katika kulifanya taifa kuwa moja lenye kufurahiwa na kila Mtanzania, Rais Samia amekuwa ameziweka nguzo hizo katika falsafa ya "R" nne, ambazo ni Maridhiano (Reconciliation), Ustahamilivu (Resilience), Mageuzi (Reforms) na Ujenzi Mpya (Rebuild).

Mwenye macho haambiwi tazama. Kila Mtanzania amejionea mwenyewe namna Rais Samia anavyoendelea kufanya maridhiano katika nyanja ya siasa ambapo kwa nyakati tofauti amekutana na viongozi wa vyama vya siasa.

Kupitia Maridhiano amekutana na viongozi wa vyama vya siasa na kufanya nao mazungumzo yenye lengo la kujenga na kuleta maridhiano na umoja wa kisiasa nchini.

Miongoni mwa viongozi aliokutana nao ni pamoja na Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe mara tu baada ya kutoka mahabusi mwaka juzi alikokuwa akikabiliwa na kesi.

Pia Rais kwa nyakati tofauti alikutana na viongozi wa vyama vya ACT Wazalendo, Chama cha ADC, Chama cha Wananchi (CUF) na pia viongozi wa Kituo cha Demokrasia Tanzania (TCD).

Katika mikutano yote hiyo, Dk. Samia alikuwa akisisitiza umuhimu wa kushirikiana ili kuijenga Tanzania yenye kuaminiana na kuheshimiana kwa misingi ya haki na kusahau yaliyopita.

Akizungumza kuhusu suala la maridhiano, Mwenyekiti wa Chadema, Mbowe alielezea umuhimu wa kuondoa uhasama wa kisiasa pamoja na kusameheana.

"Umeonesha njia kwa taifa lako namna tunavyopaswa, Rais Samia na falsafa ya R nne katika kuijenga nchi yetu Tanzania, kusameheana na kwa pamoja tujenge taifa lenye uhuru, haki, demokrasia, na maendeleo ya watu wote," alinena Mbowe.

Naye Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye akizungumzia mageuzi yanayofanywa na Dk. Samia anasema Rais amerekebisha mapungufu ya awamu zilizopita na kuyataja baadhi ya mageuzi anayoyafanya ni pamoja na kuondoa kodi za uonevu kupitia mifumo ya hakijinai, kuimarisha uhuru wa kujieleza na kurejesha haki ya kufanya mikutano ya siasa na watu kukusanyika.

### MIRADI YA KIMKAKATI

Miradi yote mikubwa ya kimkakati iliyoanzishwa au kuendelezwa na Awamu ya Tano, naye pia anaiendeleza kwa kasi ya kimbunga huku wahafidhina wengi wakiwa hawaamini macho yao!

Mradi wa jenzi wa reli ya mwendo kasi (SGR) hayati Magufuli aliacha ukiwa chini ya asilimia 90 kati ya Dar es Salaam na Morogoro, lakini kipande hicho chini ya Dk. Samia kimekamilika, baadhi ya mabehewa yameshafika, kichwa kimoja cha mabehewa hayo (injini) kimepakuliwa mwezi uliopita bandarini na tayari kimeshaanza kufanyiwa majaribio ya safari kati ya Dar na Moro!

Ile falsafa yake ya 'Kazi Iendelee', akimaanisha kuendeleza yote mazuri ya mtangulizi wake haikuwa ya kinafiki; kwani sasa vipande vyote vilivyobaki vya mradi huo vimeshasainiwa na hivi sasa makandarasi wako maeneo ya kazi wakiwajibika.

Wakati utiaji saini wa ujenzi wa kipande cha SGR Tabora-Kigoma mwishoni mwa mwaka jana, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), Masanja Kadogosa, alisema ujenzi wa SGR katika vipande vyote unaendelea vizuri.

Kadogosa alibainisha kuwa Serikali ya Rais Samia imefanikiwa kuendeleza ujenzi huo ambao mpaka wakati ule ujenzi kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro ulifikia asilimia 97.67, Morogoro hadi Makutupora ulikuwa asilimia 91.32, Makutupora mpaka Tabora ulishafika asilimia 3.26, Tabora-Isaka (asilimia 0.49) na Isaka-Mwanza ulishafika asilimia 19.70. Kumbuka takwimu hizi ni za mwaka jana, hivyo ujenzi wa reli hiyo hadi sasa utakuwa umefika mbali zaidi.

Mradi mwingine wa kimkakati ni ujenzi wa Bwawa la Julius Nyerere (JNHPP) kwa ajili ya kuzalisha umeme wa maji ya Mto Rufiji. Wakati anazindua ujazaji maji wa bwawa hilo Desemba 22, mwaka jana, Rais Samia alisema alikuta ujenzi wa mradi huo ukiwa asilimia 37 wakati anaingia madarakani lakini mpaka alipozindua ujazaji maji ujenzi wake ulikuwa umefikia asilimia 78.68 na mkandarasi aliahidi hadi kufika Aprili mwaka 2024, mradi utakuwa umekamilika na utakabidhiwa rasmi serikalini!

Miradi mingine ya kimkakati inayoendelea kwa kasi ya kimbunga ni ujenzi wa daraja la Magufuli la Kigongo-Busisi mkoani Mwanza na ununuzi wa ndege mpya za Shirika la Ndege nchini (ATCL). Kwa upande wa ATCL ndege zimeendelea kununuliwa ikiwemo ya mizigo.

Pia Dk. Samia amefanya mengi katika hii miaka yake michache katika kuanzisha miradi mipya.

Kila la heri kwa Watanzania wote kwenye kuadhimisha hii miaka 62 ya Uhuru wa Taifa letu, mwenye macho haambiwi tazama! Mambo mengi mazuri na ya msingi kuhusu maendeleo yamefanyika bila kusahau kusimamisha demokrasia madhubuti katika awamu zote sita za viongozi wa taifa hili!

***Mawasiliano ya mwandishi wa makala haya ni 0768 888 787***

Paul Mng'ong'o
KLINIKI YA FIKRA
Simu: 0676055444 Email: mngongopaul@yahoo.com

# Mambo ambayo watu wenye nguvu ya akili hawayafanyi-5



LEO ni siku nyingine. Tumshukuru Mungu kwa kutubariki kuiona siku hii.

Katika makala iliyopita ilimalizika kwa kuangalia mambo mawili muhimu ambayo watu walio na busara na nguvu ya akili hawayafanyi kwenye maisha.

Mambo hayo ni kwamba hawana chuki kwa mafanikio ya wengine na kwamba hawakati tamaa baada ya kushindwa.

Mambo mengine tuliokwisha angalia katika mfululuzi huu ni kwamba watu hawa hawatumii muda wao mwingi kujadili na kutafakari mambo yaliyopita, badala yake huwaza ya mbele. Lakini pia tukasema hawafanyi makosa yaleyale tena na tena,

Katika makala za nyuma zaidi, tuliorodhesha na kufafanua pia mambo ambayo watu walio na busara na nguvu ya akili hawayafanyi kwenye maisha.

Kwamba mtu anapoamua kuyaacha mambo hayo ndiyo kunasababisha asonge mbele kwa haraka.

Lakini bahati mbaya sana ni kwamba, wenye nguvu ya kuyaacha haya miongoni mwetu ni wachache.

Wengi wanashindwa kuyaacha mambo haya na kujikuta wakiendelea kuishi maisha ya chini siku zote.

Baadhi ya mambo mengine ambayo tumeshayataja ni pamoja na kwamba wenye nguvu ya akili hawapotezi muda kwa kujionea huruma kwa kufikiria majanga, mikosi na mitihani ya maisha inayowafika bali kusopnga mbele. Lingine tumeona ni nguvu zao kutowapa wengine kwa maana ya kutotunza hasira, chuki au kulipa visasi.

Pia tuliona kwamba watu wenye nguvu ya akili hupenda hufanya mabadiliko chanya kwa maana ya kuwa tayari kubadilika wakishaamini kwamba jambo fulani lina faida kwao kama vile kufanya mazoezi au kudumu na ibada. Hawaishii kutamani tu moyoni kwamba nitafanya kesho, nitafanya kesho na kesho kuzaa kesho bali hufanya kweli mara moja.

Pia tuliona kwamba watu wenye nguvu ya akili hawahangaishwi na vitu wasivyoweza kuvidhibiti, hawahangaiki kwa ajili ya kuwapendeza watu wote na pia hawaogopi kuamua na kuchukua hatua.

Leo tunaendelea na mambo mengine ambayo watu wenye nguvu ya akili ama huyafanya kama yana matokeo chanya au hawapotezi muda kuyafanya.

Haya ni jambo la 11, 12 na 13.

11. Huwa na muda wa kukaa pekee yao Mateso mengi ya mwanadamu hutokana na kutokujua kukaa kimya pekee.

Kutumia muda wa kutosha ukiwa peke yako si kipaumbele wala jambo la muhimu kwa watu wengi. Watu wengi hawajui umuhimu wa kutenga muda kuwa wenyewe.

Wengi wanaona kana kwamba muda mwingi wa siku wanakuwa wenyewe na wanawaza mambo mengi na kufanya kazi. Lakini leo nataka ujue kuwa watu wanaojua, wenye busara na hususani wenye nguvu ya akili, wanaupanga muda wao na kuhakikisha kuwa kila baada ya kipindi fulani wanapata nafasi hizi adhimu za kuwa mahali peke yao kwa utulivu wa kutosha.

Ndani ya muda huu, huwa mahali ambapo wanajua hawatapata usumbufu kuona watu wakipitapita au wakiwafuata kuongea nao. Hutenga eneo maalumu, huweka mbali simu zao, huzima redio, Tv na kila kitu kisha hubakia wao, mawazo yao, peni na diary. Fikra kwamba kuwa pekee ni mbaya na kuwa katika kundi la watu ni jambo zuri inatufanya tuhakikishe kuwa kila mahali tunakuwa na watu wanatuzunguka.

Kuwa na muda wa peke yako mara nyingi huchanganywa na kuwa na hisia za upweke. Lakini kuwa pekee haimaanishi upweke. Mtu anaweza kujisikia mpweke hata akiwa amezungukwa na watu.

Upweke ni hali ya kuona kwamba hakuna mtu ambaye yupo kwa ajili yako.

Lakini kuwa peke yako ni suala la kuamua na kutenga muda kwa ajili yako ili kutoa nafasi ya makusudi kwa mawazo yako kufanya kazi.

Kuna faida kubwa za kuwa kutafuta na nafasi ya peke yako. Faida kubwa ya jambo hili ni kukuamsha hisia za uamsho wa ndani, kujitathmini, kukuibulia ubunifu ambao usingeupata ukiwa na watu, kutafuta suluhu ya mambo magumu na zaidi sana kukupa nafasi ya kuibua malengo makubwa na mikakati ya maisha.

> Lakini leo nataka ujue kuwa watu wanaojua, wenye busara na hususani wenye nguvu ya akili, wanaupanga muda wao na kuhakikisha kuwa kila baada ya kipindi fulani wanapata nafasihizi adhimu za kuwa mahali peke yao kwa utulivu wa kutosha.

Nyakati hizi zinapatikana kwa kuweka mbali simu ukiwa umezima kila kitu kisha kukaa peke yako kukiwa kimya, kuendesha gari imezimwa redio au kutembea peke yako ukiwa kimya.

12. Hawajihesabu kuwa bora kuliko wengine

Sisi sote tuna uhitaj unaofanana na tuna haki sawa hapa duniani. Hisia za kuona kana kwamba wewe una haki zaidi au kama vile wewe ndiye unayetazamwa zaid au unaona kama unatakiwa kufanikiwa zaidi ya wengine n hisia zisizo na afya kwako.

Watu wenye nguvu ya akil mara zote wana utulivu, n wanyenyekevu, wanapanga mambo yao taratibu na hawajioni wao ni bora kuliko wengine.

Ukiwa na mtazamo huu inakupa utulivu zaidi na utafanya mambo yako kwa utulivu wala hutakuwa na mzigo wa kuwaonesha watu kuwa wewe ni bora sana Hali hii itakupa nafasi nzur kuchagua njia zako na kufanya vizuri bila msukumo wowote wa kihisia.

13. Hawatarajii matokeo ya haraka Watu wote wenye nguvu ya akili wanaamin juu ya mipango, utekelezaj wa mipango, wanaamini juu ya makosa na marekebisho ya makosa na zaidi sana kwenye kila wanachokifanya wanatambua suala muda uvumilivu, jasho kwa maana ya juhudi na kusubiri.

Watu hawa pia kabla ya kufikiria au kutamani matokeo ya haraka wanatambua uwepo wa Mungu na mapenzi yake kwenye maisha yetu, kwa maana nyingine wanaomba Mungu na kuruhusu mapenzi yake kuchukua nafasi.

Hivyo ni mbaya sana kuishi kwa kutegemea tu matokeo ya haraka. Hali hi inaweza kukusababishia kuchanganyikiwa zaidi kwa sababu wengi wanaotaka matokeo ya haraka huishia kuvurugikiwa na kupoteza matumaini baada ya matarajio yao kuchelewa au kutotimia.

Ni vizuri kuwekeza kwenye hatua huku tukijua kuwa mwelekeo siku zote ni muhimu kuliko kasi (Direction is better than speed).

Makala hii inaishia hapa na wakati ujao tutaanza makala nyingine.

**Wework Consult - Your Partner in Growth.**

# Nyerere na safari ya kudai uhuru

## ● Kassela Bantu alimkutanisha na 'Waswahili' wa Dar

**Na Hamid Yassin**

KWA mujibu wa vyanzo mbalimbali, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alikuja rasmi Dar es Salaam mwaka 1952 kwa ajili ya kufundisha Shule ya Mtakatifu Francis, siku hizi Pugu.

Alikuwa tayari amekutana na Hamza Mwapachu huko Tabora mwaka 1945, na kisha kwenda chuoni pamoja Makerere Uganda na baadaye nchini Uingereza kuchukua masomo ya juu.

Akiwa masomoni na Mwapachu, Mwalimu Nyerere alianza kusikia harakati za chama cha TAA, pia alihadithiwa habari za mwanaharakati Abdulwahid Sykes kupitia kwa Mwapachu.

Waliporudi kutoka Uingereza, Mwapachu na Nyerere walirejea Tabora ambako Mwalimu alikutana na Kasella Bantu katika shule ya St. Mary's School, siku hizi Milambo, walipofundisha pamoja.

Kasela Bantu alikuwa mwanachama wa TAA mwenye msimamo mkali katika kupinga ukoloni.

Mwalimu katika hotuba ya kuaga, aliyoitoa Novemba 5 mwaka 1985 kwa Wazee wa Dar es Salaam, aliwataja watu waliomuunga mkono kabla na baada ya kuundwa kwa TANU na hatimaye kudai uhuru.

Alisema kwamba alikuwa Kasella Bantu aliyemtambulisha kwa Abdulwahid Sykes ambaye wakati huo alikuwa Rais wa Chama cha Tanganyika African Association (TAA).

Hii ilikuwa ni moja ya zile nyakati adimu ambazo Mwalimu Nyerere alizungumza hadharani kuhusu siku zake za mwanzo za kiharakati na kisiasa.

Mwalimu Nyerere alisema kwamba alikuwa mgeni Dar es Salaam na kwamba Kasella Bantu ndiye aliyemtambulisha kwa Abdulwahid na kisha kumkutanisha na watu maarufu wa Dar es Salaam.

Mbali na Dossa Aziz aliyekutana na Nyerere kwa muda mfupi katika mkutano mkuu wa TAA Aprili 1946, Kasella Bantu mwenyewe na Denis Phombeah, hakuna mtu mwingine pale Makao Makuu ya TAA aliyekuwa akimjua Mwalimu Nyerere.

Abdulwahid, Mwalimu Nyerere, Ally Sykes, Dossa Aziz, Stephen Mhando, John Rupia, Dunstan Omari na wengine walizoea kukutana kila Jumapili kwa ajili ya mazungumzo nyumbani kwa Dossa Aziz, mtaa wa Congo au nyumbani kwa Abdulwahid mtaa wa Stanley. Sehemu hizi ndizo ambazo wazalendo hawa walikuwa wakikutana kujadili mustakabali wa Tanganyika.

Midahalo ya kisiasa miongoni mwa wazalendo hawa, wakati huo wakiwa vijana, ilihama kutoka mada za manung'uniko ya ndani ya nchi hadi kutafuta njia ya kupata uhuru na masuala ya kimataifa ya mrengo wa kushoto yahusuyo serikali na maamuzi binafsi ya Waafrika wenyewe.

Inaelezwa kuwa, Mwalimu Nyerere alimwona Abdulwahid kuwa ni mtu mwenye akili sana, asiye na choyo na mtu wa kupendeka. Kwa upande mwingine Abdulwahid naye alimwona Nyerere kuwa ni mtu aliyeelimika na mwenye uwezo wa uongozi.

Wakati huo tayari Mwalimu Nyerere alishapata nafasi ya kuifahamu dunia vizuri na kutiwa bidii kwa siasa za Fabian Society wakati alipokuwa mwanafunzi nchini Uingereza.

Chama cha Wafanyakazi cha African Association kiliposhiriki katika ule mgomo wa jumla wa mwaka 1947 kule Tabora, Mwalimu Nyerere hakujihusisha na chama hiki cha wafanyakazi ingawa alikuwa katibu wa chama hicho.

Kutokana na sababu hiyo kuheshimiana kulitokea baina ya Abdulwahid na Nyerere. Kila Jumapili Nyerere alikuwa akisafiri kutoka Pugu alipokuwa akifundisha katika Sekondari ya Pugu hadi Dar es Salaam kuhudhuria mikutano hii isiyokuwa ya kawaida.

Baada ya mikutano ama Dossa Aziz au Dunstan Omar alimrudisha Mwalimu Nyerere kwa gari hadi Pugu. Hivi ndivyo Mwalimu Nyerere alivyokuja kuingia ndani ya duru za ndani zaidi za TAA katika makao makuu na hatimaye akaja kupendekezwa kugombea cheo cha juu kabisa cha uongozi wa chama, Aprili, 1953.

Uongozi wa TAA ulimpendekeza Mwalimu Nyerere ili kukiimarisha chama kutokana na kuwa Mwafrika aliyekuwa amesoma vizuri.

Ilibakia kwa yeye mwenyewe kulikubali au kulikataa shauri hilo; kabla yake Chifu Kidaha Makwaia alishauriwa kuchukua uongozi wa TAA ili kuchukua urais lakini alilikataa.

Nyerere alikuwa mwalimu aliyefundishwa na Wakatoliki wa Roma na alipitia mfumo huo ambao uliwafanya walioupitia wawe watiifu na waaminifu kwa vyote viwili; kanisa na serikali!

Vilevile Mwalimu Nyerere alikuwa chini ya ushawishi wa Padri Richard Walsh aliyemsaidia Mwalimu kusoma nchini Scotland. Kumbuka wakati ule taasisi za dini na mamlaka za kikoloni zote zilikuwa adui wa siasa za Kiafrika!

Inasemekana kwamba Padri Walsh alikuwa na ushawishi wa kutosha juu ya maisha ya Mwalimu Nyerere kwani alimlea na alimfanya ajiunge Chuo Kikuu cha Edinburgh, hivyo haikuwa rahisi kwamba aje kuipinga serikali ya kikoloni.

Mwalimu Nyerere alitarajiwa abakie kwenye kazi ya ualimu katika shule yoyote nchini Tanganyika.

Kumbuka Mwalimu Nyerere alikuwa ndio kwanza amerudi toka masomoni nchini Uingereza mwaka mmoja nyuma na alikuwa anataka kutulia aanze maisha, lakini wale 'vijana wa mjini' aliowakuta tayari wameanza harakati za kisiasa mjini Dar es Salaam kama Abdulwahid, mdogo wake Ally, na Dossa Aziz huku wakiwa matajiri wakiishi ndani ya mazingira yao wenyewe, ilikuwa chachu muhimu kwake kugeukia siasa.

Kidole kimoja hakivunji chawa, Mwalimu Nyerere alijua yeye kama yeye kamwe asingeweza kujenga msingi wa kisiasa katika mazingira ya Dar es Salaam ya miaka ya 1950 ambako siasa ilichukua tabia za dini hususani ile ya Kiislamu. Mwanzoni Mwalimu Nyerere hakutaka kulikubali shauri hilo la kuwa kiongozi wa TAA.

Uongozi wa chama cha TAA ulielewa na kutambua thamani ya elimu ya Mwalimu Nyerere na uwezo wake kwa uongozi wa baadaye wa chama na nchi yenyewe.

Abdulwahid pamoja na watendaji wa TAA waliamini kwamba kuwa na mwafrika aliyeelimika kama rais wa chama kungeimarisha uongozi wake na kutoa sura nzuri machoni pa serikali ya kikoloni.

Mwalimu Nyerere alipata kusema kwamba, ilikuwa nia yake kufundisha kwa muda kisha aingie kwenye siasa. Hatimaye alikubali ule uongozi ambao TAA ilipanga kumpa.

Nje ya duara la uongozi wa TAA ambao ulimpendekeza kugombea, Mwalimu Nyerere alikuwa mgeni kabisa kwa wote waliokuwa na haki ya kupiga kura, lakini alishinda uchaguzi ule!

TAA ya Abdulwahid, Ally, Dossa Aziz na Rupia lilikuwa tayari imekwishaamua kumfanya Mwalimu Nyerere awe rais wa chama.

Mwalimu Nyerere alianza kazi ya kuiongoza TAA kwa gia kubwa zaidi kwa kuimarisha harakati za kudai uhuru kutoka kwa Waingereza.

Aliongoza TAA hadi mwaka 1954, walipoboresha katiba yao na kufikia Julai 7 mwaka huo (1954) chama kilibadilishwa jina rasmi kutoka TAA na kuwa Tanganyika African National Union (TANU) huku lengo kuu la chama hiki ikiwa ni kudai uhuru kamili wa Tanganyika.

Madhumuni mengine ya TANU yalikuwa ni pamoja na kuudumisha uhuru wa nchi na raia wake, kuweka heshima ya mwanadamu kwa kufuata barabara kanuni za Tangazo la Ulimwengu la Haki za Binadamu, kuhakikisha kwamba nchi yetu inatawaliwa na serikali ya watu ya kidemokrasia na ya kisoshalisti.

Pia kushirikiana na vyama vyote vya siasa katika Afrika vilivyokuwa vinapigania uhuru wa bara lote la Afrika, kuona kwamba serikali inatumia mali yote ya nchi yetu kwa kuondoshea umaskini; ujinga na maradhi, inasaidia kwa vitendo kuunda na kudumisha vyama vya ushirika, kila iwezekanapo inashiriki hasa katika maendeleo ya uchumi wa nchi.

Malengo haya ya TANU hayakubaki kwenye maandishi tu, bali yalishinikizwa kwa Serikali ya Kikoloni ya Uingereza na taratibu walianza kuipata 'joto ya jiwe' kwani walimwandama Mwalimu Nyerere usiku na mchana ili wamshitaki na ikiwezekana wamfunge jela!

Pia hii ilimponza kwa kupoteza marafiki zake kadhaa, lakini pia alikuwa amejitia matatani dhidi ya wakoloni wa Kiingereza waliokuwa wanaitawala Tanganyika wakati huo.

Serikali ya Kikoloni iliyokuwa ikiongozwa na Gavana Richard Turbull, ilimshtaki Mwalimu Nyerere kufuatia makala yake aliyoandika kwenye gazeti la 'Sauti ya TANU' la Mei 7 mwaka 1958 ambayo alidai baadhi ya wakuu wa wilaya walikuwa wanatumiwa na wakoloni hao kuihujumu TANU. Kumbuka wakati huo wakuu wa wilaya wote walikuwa ni wazungu!

Agosti 13 mwaka 1958 Mwalimu Nyerere alikutwa na hatia ya mashtaka mawili ya kuwaita watawala wa kikoloni 'washenzi na maharamia'. Alitozwa faini ya Sh. 3000 au kwenda jela miezi sita na kupewa siku mbili za kulipa faini hiyo. Alilipa faini.



*Mawasiliano ya mwandishi 0768 888 787*

# Umasikini na maendeleo ya Tanzania - 4

**Na Dk Felician Kilahama**

MUNGU ni mwema. Leo tunakutana katika sehemu ya nne ya makala hii kuhusu umasikini na maendeleo ya Tanzania.

Tumeingia sehemu hii leo Desemba 9 tukiadhimisha miaka 62 ya uhuru wa nchi yetu na huku mapambano dhidi ya umaskini yakiendelea.

Katika sehemu ya tatu, ilihitimishwa kwa kuainisha kwamba Tanzania, kwa mtazano wa nchi tajiri, inaonekana ni taifa maskini. Tukasema huu siyo mtazamo sahihi hivyo ni wajibu wetu kuonesha kwa vitendo kuwa Tanzania ni taifa tajiri na watu wake ni matajiri wanaoishi kwa furaha na amani katika hii miaka 62 ya uhuru.

Kwa mtazamo wangu, Watanzania hatuna budi kujizatiti kuendelea kuujenga uwezo wetu wa ndani tukijua kuwa maendeleo ya kweli kwa Tanzania nzima yatatokana na sisi watanzania wenyewe.

Katika sehemu ya kwanza ya mfululizo wa makala haya, nilifafanua kuwa mataifa yaliyoendelea hayakulaza damu; wananchi wake zaidi ya miaka 300 iliyopita, walidhamiria kwa dhati wakajiletea maendeleo ambayo kizazi cha sasa kinajivunia.

Hata kama mataifa tajiri yameboresha zaidi tekinolojia na kuongeza ufanisi; hali hiyo haikujitokeza kirahisi. Kumekuwepo na jitihada za makusudi zilizofanywa na mababu wao tangu miaka ya nyuma walipoona umuhimu wa kuja Afrika na kukusanya rasilimali na kuzichukua kadri walivyoweza.

Hivyo wakadiriki kuendeleza kwao kiasi cha kujiletea maendeleo ikiwemo viwanda na tekinolojia mbalimbali.

Hivyo, tunapokaribisha wawekezaji siyo kwamba mitazamo/fikra vimebadilika bali tujue kuwa wanakuja kufanya biashara ili wanufaike zaidi kupitia faida watakazopata.

Hii ni sawa, wapate faida lakini wanapotumia rasilimali tulizonazo, kuwepo na msingi mzuri wa Watanzania pia kunufaika kwelikweli. Yaani wakinufaika tunufaike pia (win-win situation). Wasichume na kuondoka huku wakituacha tumedhoofika. Kama ni madini, yakiisha watatuachia mashimo lakini faida tutakayobaki nayo iakisi uwezo wa kufukia hayo mashimo na bado tukabaki na faida maradufu.

Tukumbuke kuwa, wakati mwingine, historia hujirudia hivyo wanapopata fursa za uwekezaji watakuja na mawazo ya kunufaika zaidi kupitia rasilimali au malighafi zetu kuendeleza zaidi huko walikotoka.

Hivyo, tusipokuwa makini tutatawaliwa wakati sisi ndiyo wenye rasilimali muhimu na wakati mwingine tukisingizia hatuna uwezo wa kuzitumia.

Hivyo tuwe macho na faida itakayohamishiwa nje ya nchi kupitia ukoloni-mamboleo.

Kimsingi, sikatai dhana ya uwekezaji lakini wawekezaji wa kwanza kupewa kipaumbele ni vyema wawe Watanzania. Hakuna linaloshindikana kama wao waliweza na sisi tutaweza, kinachotakiwa ni utashi madhubuti wa kisiasa kwa msingi wa kulipa msukumo wa juu suala hili muhimu, tutaiendeleza Tanzania.

Wawekezaji kutoka nje wafanye hivyo kwa ubia na Watanzania kwa nia njema ya kuziba mapengo si mapungufu katika sehemu ambazo kuna umuhimu sana wa kufanya hivyo kulingana na mipango mahususi ya taifa ya muda mfupi na mrefu.

Dhamira iwe njema ya sisi kujiimarisha kimaslahi (taifa na watu wake) lakini pia kujijengea uwezo halisi wa kujitegemea kwa asilimia kubwa. Tujue tangu awali tunahitaji uwekezaji wa namna gani kwa faida ya Watanzania wote.

Ili taifa lifanikiwe lazima kujizatiti kwelikweli ikiwa ni pamoja na kuhakikisha sera za uchumi na maendeleo ya Watanzania, zinatanguliza utaifa kuliko ubinafsi na tuondokane na mitazamo potofu kwa watu wachache kutaka kujilimbikiza mali kwa kupindishapindisha sera na maamuzi.

Viongozi kwa ngazi zote wawekeze zaidi kwenye 'uzalendo kuliko mawazo binafsi na wazingatie maadili mema, mathalani, alivyokuwa Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere ambaye namwangalia kama kioo kikuu cha jamii ya Watanzania.

Hebu tujitathimini ipasavyo, tujue nini vikwazo na tuvishughulike ipasavyo. Hakuna linaloshindikana tunaweza: iwapo siasa safi zipo, ardhi toshelezi ipo, utajiri asilia tunao, nguvukazi ya kutosha ipo kinachotakiwa ni kuwepo na uongozi bora na makini.

Hivyo, ili taifa lifikie maendeleo tunayoyakusudia lazima yafanyike maamuzi sahihi na uwekezaji stahili na makini.

Serikali imerejesha Wizara ya Mipango maanake nini? Ni kuwa na chombo madhubuti cha kupanga na kusimamia maendeleo ya Watanzania. Kadhalika, ni muhimu kuwa na dira ya kitaifa iliyosheheni maono makubwa ya muda mfupi na mrefu ili kufanikisha nia ya kuwa na taifa lenye uchumi imara.

Vilevile, ni muhimu kukawepo na kikundi maalumu (think-tank) cha taifa (ndani ya Tume ya Taifa ya Mipango?) ambacho kazi yake kubwa itakuwa kuibua maono muhimu yatayokubaliwa kitaifa; na hatimaye kutafsiriwa kwenye mipango ya utekelezaji ya muda mfupi na mrefu.

Katiba itakayopitishwa iwe ndiyo msingi wa taifa kujiletea maendeleo-endelevu na mipango mizuri iwe chachu ya kuinua kipato cha Watanzania na pato kuu la taifa.

Rasilimali tunazo, tena za kutosha hivyo tujiimarishe kiutendaji na katika stadi za kazi mbalimbali kwa lengo la kuinua uchumi wetu; mtu mmojammoja na hatimaye taifa zima.

Hata hivyo, tuzingatie umuhimu wa uzalendo, upendo na kutokukumbatia ubinafsi; tuondokane na ubadhilifu wa fedha na mali za umma.

Tulipopata uhuru wananchi walikuwa na moyo wa kufanyakazi pamoja kujiletea maendeleo. Miundombinu ya shule, zahanati, hata barabara kupitia jamii husika kwa njia ya 'msalagambo', yaani kujitolea ilijengwa. Mengi yalifanyika kwa sababu utashi wa kisiasa ulikuwepo. Tufufue hali hiyo.

Mtazamo umekuwa zaidi kupata rasilimali fedha kutoka nje (kukopa au misaada) jambo ambalo ni sawa lakini swali ni tunakopa kufanya kitu gani? Sikatai kukopa kwa sababu wakati mwingine ni muhimu sana lakini tujipangie mambo ambayo tunaweza kuyafanya kwa kutegemea uwezo wetu wa ndani (nguvu;kazi, rasilimali-fedha na maliasili zilizopo) tuyafanye bila kutegemea mikopo.

Watanzania asilimia takribani 75 wanaishi vijijini na kiutendaji wanahudumiwa zaidi na serikali za mitaa kupitia halmashauri za wilaya.

Tangu taifa liingie kwenye mfumo wa halmashauri takribani miaka 40 imepita; hali ya maendeleo vijijini katika baadhi ya maeneo imekuwa hairidhishi sana hususani katika masuala ya huduma za jamii na miundombinu.

Mathalani, katika sekta ya elimu wanafunzi wamekuwa wakiongezeka kwa idadi lakini miundombinu ya madarasa pamoja na madeski imekuwa haikidhi mahitaji halisi. Hali hiyo imekuwa ikipelekea wanafunzi kujazana kwenye chumba kimoja au kukaa chini kwa kukosa madeski.

Kwa upande mwingine sera, sheria na mikakati husika havijawa rafiki kiasi cha kuziwezesha halmashauri zote kutimiza wajibu wake ipasavyo. Mathalani, ukidadavua bajeti kuhusu fedha za maendeleo ambazo zimekuwa zikitengwa na kutolewa kwa halmashauri nchini; ukalinganisha na kiasi ambacho kimekuwa kinatolewa kwa wizara zote na taasisi zake; utaona tofauti kubwa sana.

Iwapo tungepata takwimu za miaka 40 iliiyopita (1982 mpaka 2023) matrilioni mengi sana ya fedha yataonekana kutumika katika serikali kuu ukilinganisha na kiasi kilichotengwa na kutumika katika serikali za mitaa ambako ndiko waliko Watanzania wengi.

Iwapo kusudio ni kuongeza kiwango cha kipato kwa Watanzania wengi; pamoja na kuendeleza na kuimarisha huduma za kijamii vijijini; kujenga na kuendeleza miundombinu imara kama barabara, umeme, mabwawa ya umwagiliaji, masuala ya elimu, afya; na kwa kuzingatia umuhimu wa kuimarisha utendaji katika serikali za mitaa; picha ambayo ingeonekana ni bajeti kubwa kwenda kwa halmashauri kwa maono yangu kuliko serikali kuu.

Kiuhalisia halmashauri zimekuwa zikichechemea katika kutekeleza majukumu yake kutokana na kutowezeshwa ipasavyo. Ukiweka kando bajeti inayotengwa pia 'kitendawili' kipo kwenye upatikanaji wa fedha zilizotengwa. Uzoefu unaonesha kuwa imekuwa vigumu kuzipata kwa wakati na kwa kiasi kilichokusudiwa.

Kadhalika, halmashauri hazina wataalamu wa kutosheleza mahitaji karibu katika sekta zote. Ukilinganisha na wizara au taasisi husika. Uzoefu unaonesha kwamba serikili kuu imebeba wataalamu wengi, kutengewa fedha zaidi na kupatiwa vitendeakazi vingi kuliko halmashauri, mfano, magari, vifaa ofisini na fedha.

Kwa kuwa nia yetu ni kuharakisha maendeleo huko vijijini na mijini tubadilike kifikra na kuongeza nguvu kwenye halmashauri na taasisi zinazoshughulika na masuala muhimu ya wananchi (vijijini na mijini) mathalani, vyama vya ushirika, SACCOS na kadhalika.

Imani yangu ni kwamba hata majukumu ya serikali kuu, mengi yanaangukia huko halmashauri zilipo. Hivyo, badala ya kutawanya nguvu ni bora kuunganisha nguvu kwa faida ya wote na kuhakikisha utekelezaji wa mipango husika unafanyika kwa ufanisi mkubwa na kuharakisha mapinduzi katika shughuli za kijamii vijijini na mijini.

Nashauri serikali za vijiji na mitaa mijini ziimarishwe kuliko ilivyo sasa. Viongozi wake wawe ni wenye upeo na uwezo mkubwa wa kusukuma maendeleo kwenye maeneo wanayoyasimamia.

Nashauri kuwepo na mfumo rasimi wa utawala na uongozi kwenye ngazi hizo na masilahi yao yasipuuzwe. Kwa kufanya hivyo tunaweza tukayapima mafanikio yetu kupitia vigezo tutakavyojiwekea.

*Itaendelea*



# Wimbo wa 'wamemiliki sana mpira zaidi yao' sasa unachosha wacheze kwa malengo







> Yanga isiwe inasifiwa tu bali iwe inashauriwa yaliyo bora ya kufanya ili isikwame kwenye malengo makubwa. Wimbo wa "wamemiliki sana mpira kuliko wapinzani wao," sasa umechosha na wala hauna tija.

**Na Ibrahim Mkamba**

SHUKRANI sana kwa goli la kusawazisha la Pacome. Pointi moja si mbaya kwa mechi ya pili ya ligi ya mechi sita. Jamii yetu inafanya juhudi kubwa kuipandisha juu Yanga kwa kila inachofanya. Mashabiki tunafurahi sana kwa hilo lakini hilo haliisaidii Yanga. Sasa hivi jamii inaficha udhaifu wa Yanga kwa hoja ya "wamemiliki sana mpira zaidi ya wapinzani wao licha ya kutopata matokeo mazuri." Mashabiki tunafurahi sana ikielezwa hivyo lakini mambo hayaendi.

Ni vizuri Yanga wakiambiwa wazi kuwa mafanikio kwenye mashindabno makubwa ya timu kubwa tupu hutokana na si kumiliki sana mpira peke yake bali na mipango mingine ya umakini mkubwa kiuchezaji.

Tusifikie mwisho wa ligi hii hatua ya makundi na kukosa kwenda robo fainali huku tukifurahia sifa ya "wamekwama kwenda robo fainali lakini wamemiliki sana mpira mechi zote kuliko wapinzani wao wote". Itasaidia nini hiyo wakati hao ambao hawakumiliki sana mpira wameenda robo fainali?

Yanga isiwe inasifiwa tu bali iwe inashauriwa yaliyo bora ya kufanya ili isikwame kwenye malengo makubwa. Wimbo wa "wamemiliki sana mpira kuliko wapinzani wao," sasa umechosha na wala hauna tija. Timu zetu zote za Yanga na Simba zina nafasi kubwa ya kwenda robo fainali. Tuwasaidie badala ya kuwapambapamba.




Kuhusu mchezaji wa siku kama ni kweli kocha amesema havutiwi na mechi kupewa majina ya wachezaji wake, naamini sababu itakuwa anaiona hiyo kama njia ya siku moja kulazimishwa amchezeshe mchezaji ambaye hakuwa na mpango wa kumchezesha siku hiyo.

Hebu tutafakari mfano huu. Kocha ana mabeki wazuri tupu wanne wa kati. Kwa kumsoma mpinzani, kwa mipango yake, kwa utendaji kwenye mazoezi kaona wawili fulani na fulani ndiyo wangefaa kwa mechi hiyo. Kwa bahati mbaya aliyetajwa kuwa ndiye mwenye mechi si miongoni mwa ambao kocha alipanga kuwatumia kwa mechi hiyo.

Hapo moja kwa moja atakuwa amelazimishwa amtumie kinyume na sababu zake za kiufundi. Akiwa jasiri kusimamia mipango yake bila kumtumia mchezaji huyo, atakuwa ameanzisha mgogoro mkubwa ajabu na watu wengi wa klabu wakiwemo viongozi, wanachama na mashabiki.

Kweli, utaratibu huu inabidi utazamwe kwani unakuwa kama namna ya kumshinikiza kocha afanye ilivyopangwa na uongozi wa klabu. Ni kama njia fulani ya kumuingilia kocha kwenye kazi yake.

# Kutoka katika umaskini hadi utajiri kisa soka

**Na Valensi Mbaga**

SOKA ni eneo ambalo limewapa kila mtu kutoka nyanja mbalimbali nafasi ya kupambana na umaskini na kuishi maisha ambayo alikuwa anayatamani. Ingawa wachezaji hao wamethibitisha kuwa vipaji ni njia ambayo Mungu amewapa ili kujinasua na umaskini, sio tu kwamba wameepuka janga hilo bali wamekua miongoni mwa watu matajiri zaidi duniani. Soma makala hii na ujue japo kuhusu wanasoka watano tu waliotoka kwenye umaskini na kupanda ngazi hadi kwenye utajiri mkubwa.





**1. Diego Armando Maradona**

Maradona anayejulikana kama mwanasoka bora zaidi katika historia, alizaliwa katika Villa Fioriotio, tarehe 30 Oktoba 1961. Waliishi katika makazi duni ya Villa Fiorito nje ya Buenos Aires, lakini Maradona bado angejiona kama mchezaji mzuri wa kandanda. Baba yake Don Diego alijitahidi kama fundi matofali na mfanyakazi wa kiwanda kulea watoto saba na mke wake aliekuwa mama wa kukaa nyumbani tu.

Maradona bado alisukuma ufundi wake uwanjani na alifanikiwa kusaini mkataba wake wa kwanza wa kitaalamu akiwa na umri wa miaka 15 na kusaidia familia yake.Baada ya hapo alikuwa na kazi nzuri na akiwa na umri wa miaka 21, alijiunga na Barcelona kwa ada iliyovunja rekodi ya dunia.

Maradona alifariki Novemba 2020 akiwa na umri wa miaka 60 kutokana na mshtuko wa moyo.

**2. Cristiano Ronaldo**

Cristiano Ronaldo ni mwanasoka wa kulipwa wa Ureno kwa sasa anachezea klabu ya Ligi ya Wataalamu ya Saudi akiitumikia Klabu ya Al Nassr.

Wengi wanajua mafanikio yake kama mmoja wa wanasoka bora wa wakati wote, lakini sio wengi wanaojua kuwa ni mmoja wa wanasoka kutoka asili duni.

Alilelewa katika mtaa maskini katika nyumba ya Wakristo Wakatoliki huko Santo Antonio, Ureno. Baba yake alikuwa mlevi huku mama yake akiwa na wakati mgumu kulea watoto wanne.

Kwa upande mwingine, alikuwa mvulana aliyejaa ndoto. Alipoenda shule lakini alifukuzwa akiwa na umri wa miaka 14 baada ya kumrushia kiti mwalimu ambaye hakumheshimu. Hata hivyo alitaka kutafuta kazi kusaidia familia lakini mamake alikataa na kumtaka afuate ndoto yake kama mwanasoka.

Hii ilikuwa mafanikio ya Cr7 kubwa ambayo sasa inatikisa ulimwengu wa soka. Kufikia 2023, Forbes inakadiria utajiri wake kuwa dola milioni 500, na kumfanya kuwa mmoja wa wanasoka matajiri zaidi ulimwenguni.


**3. Zlatan Ibrahimovic**

Zlatan Ibrahimovic ambae kwa sasa amestaafu soka alikuwa ni mmoja wa wachezaji wa soka ambao walikua maskini. Hakuna mtu aliyejua kuwa mvulana mwembamba, maskini, asiye na muonekano angegeuka kuwa mmoja wa wanasoka wakubwa na kupata jina la 'Simba'.

Zlatan alilelewa katika mradi hatari wa makazi katikati mwa Malmo nchini Uswisi. Utoto wake ulikuwa wa fujo na usio na malezi bora.

Wazazi wa Zlatan walitengana alipokuwa na umri wa miaka miwili, na kufanya hali yake kuwa mbaya zaidi. Hii ilimfanya aangalie maisha kwa njia tofauti na ilimbidi kuwa na nguvu na mkali ili kunusurika na ukweli mbaya wa maisha. Alifanikiwa kutoroka utumwa na kuwa mmoja wa wachezaji wanaoheshimika zaidi wakati wote.

Msweden huyo ana utajiri wa dola milioni 190. Alikuwa mmoja wa watu waliopata pesa nyingi zaidi katika kandanda na ameshirikiana na makampuni makubwa kama Nike, Volvo na H&M.



**4. Sadio Mane**

Sadio Mane ni mchezaji wa kulipwa wa Senegal anayecheza kama mshambuliaji wa timu yaAl Nassr ya Saudi Arabia . Ana umri wa miaka 31 na alikulia Bambali, mji mdogo katika wilaya ya Sédhio nchini Senegal. Kwa sababu ya historia yao, Mane hakuwahi kwenda shule na baba yake alimpiga marufuku kucheza mpira wa miguu na badala yake kuzingatia dini.

Hata hivyo aliendа kucheza na watoto katika mtaa huo. Shukrani kwa hili, skauti wa Kifaransa alimgundua na kumpeleka Ufaransa ili kuonyesha talanta yake ya ajabu na huko alianza kuchezachini ya Klabu ya watoto ya Metz.



Kazi ya Sadio Mane inaendeshwa sana na utoto wake na daima anajaribu kusaidia wahitaji katika jamii. Tofauti na nyota wengine wa michezo ambao hujivunia magari ya bei ghali, vito na mtindo wa maisha, yeye anapendelea kujenga shule na kuwapa masikini chakula na mavazi.

**5. Neymar Jr.**

Neymar ni mchezaji wa kulipwa wa Brazil ambaye kwa sasa anacheza kama mshambuliaji wa timu ya Saudi Arabia ya AL Hilal. Kazi yake ilianza katika wilaya ndogo kusini mwa Brazili, ambayo ilikuwa vizuizi vichache kutoka kwa dampo la ndani. Waliishi maisha magumu sana hata hawakuweza kumudu uchunguzi wa ultrasound kabla ya kuzaliwa kwake.

Kwa nia ya Neymar katika soka, alisaini mkataba wake wa kwanza akiwa na umri wa miaka 12, hatua iliyozifanya timu za juu kama Barcelona na Real Madrid kumtazama kwa karibu kijana huyo. Alicheza mechi yake ya kwanza akiwa na umri wa miaka 17, jambo ambalo lilimpa mwanzo mzuri wa kazi ambayo ingeweka historia katika mchezo huo.

Utajiri wa Neymar unakadiriwa kuwa dolla millioni 250 mwaka wa 2023 na ni uthibitisho wa ujuzi wake usio na kifani, ari yake na uwezo wake katika soka. Kuanzia mwanzo duni nchini Brazil hadi kuwa mmoja wa wanariadha wanaolipwa pesa nyingi zaidi ulimwenguni, safari ya Neymar ni motisha kwa wengi.s

Kwa sasa Ulimwengu wa kandanda unajumuisha baadhi ya wanasoka bora ambao ulimwengu umewahi kuwaona. Baadhi ya wachezaji walijigeuza na kuwa chapa kubwa za biashara na kuashiria mahali pao katika nafasi ya ujasiriamali. Wanasoka wenye ushawishi mkubwa zaidi ni wale waliofanya vyema kwa klabu na nchi na kufanikiwa sana katika maisha yao ya kibinafsi.







> Maradona bado alisukuma ufundi wake uwanjani na alifanikiwa kusaini mkataba wake wa kwanza wa kitaalamu...

# Msanii wa Kenya anayeumizwa na kuporomoka Hiphop Tanzania

**Na Valensi Mbaga**

BRIAN Ouko Omollo, almaarufu kwa jina la kisanii Khaligraph Jones na mara nyingi hujulikana kama Papa Jones, OG, ni rapper wa Kenya anayejulikana kwa ubora wa kazi yake na nyimbo zake kama ; Mazishi, Yego, No Change ft. Fena, Aiseee ft. Ray C,"Superwoman ft. Mr Eazi, All The Way Up , Now You Know ft. Rostam na nyingine nyingi.

**Historia yake ya maisha**

Khaligraph Jones ni mmoja wa watu wenye majina makubwa katika muziki wa Kiafrika. Alizaliwa Juni 12, 1990 huko Kayole, Nairobi, Kenya, Mama yake alimpa jina Ouko Robert kwa heshima ya marehemu mwanasiasa wa Kenya Dr. Robert Ouko, aliyeuawa tarehe 13 Februari 1990.

**Safari ya mziki**

Khaligraph alianza kurap alipokuwa darasa la 5, na shukrani kwa kakake mkubwa Span Kob ambae alimuunga mkono katika safari yake hiyo aliyoamua kuianzisha. Rapa huyo mashuhuri alifichua kuwa wimbo wake wa kwanza kutolewa ulikuwa wimbo wa injili.

Alianza kazi yake rasmi mwaka wa 2008 katika hafla iliyoitwa "Maneno na Picha Na alifanikiwa kutoa albamu yake ya kwanza ya studio ya urefu kamili Testimony 1990 mnamo Juni 2018.

**Je, Khaligraph ndiye rapper bora zaidi barani Afrika?**

Khaligraph Jones ndiye rapa anayeongoza barani Afrika. Mtazamo wake na upendo wake kwa muziki wake ulimfanya kuwa tofauti na wasanii wengine wa hip-hop wa siku hizi. Ameonyesha kuwa na nguvu na uwekezaji mkubwa kwa sababu ya nyenzo zake dhabiti na na ubora wa kzi zake.




Khaligraph Jones

**Tuzo alizoshinda**

Khaligraph Jones amepata tuzo nyingi kutokana na kazi zake. Tangu wakati alipoanza kufanya kazi hii , amepokea tuzo na tuzo nyingi ikiwa ni pamoja na Tuzo ya AFRIMA mwaka 2018 ya Best Rap Act na kuteuliwa tena mwaka 2020 kuwania tuzo mbalimbali za AFRIMA.

Alishinda pia Best Hip Hop Act kwenye Soundcity MVP Awards mwaka 2020,na Rapper wa Mwaka wa Afrika Mashariki katika tuzo ya MTN Uganda mnamo 2021 na pia uteuzi wa Tuzo za BET 2021 kwa Rapper bora wa mwaka.

**Utajiri wake**

Khaligraph Jones ndiye rapa wa nne kwa utajiri nchini Kenya, akiwa na utajiri wa dola milioni 3.8. Utajiri huo pia unajengwa na umiliki wa majumba makali na magari ya kifahari.

Khaligraph anaeshikilia nafasi ya nne , wapo wasanii wengine kama King Kaka na Abbas Kubaff ambae ni rappers wa pili na wa tatu kwa utajiri. King Kaka ana utajiri wa dola milioni 4.8, wakati Abbas Kubaff ana utajiri wa dola milioni 4

**Makazi na Familia yake**

Kunaweza kuwa na nyumba nyingi kama 100 na zaidi ya watu 500 wanaoishi katika eneo dogo. Khalighraph Jones alionekana kuish maeneo ya Pipeline akiishi katika baadhi ya mashamba ya watu wa tabaka la kati huko Eastlands, lakini leo anaishi katika moja ya mashamba makubwa ya Nairobi, Karen.

Khaligraph ni Baba wa mtoto mmoja ajulikanaye kwa jina la Amali J Ouko aliyempata pamoja na mwanadada Georgina Muteti

Mkewe Georgina ndie aliyefichua jina la binti yao kwa mara ya kwanza kwenye siku yake ya kuzaliwa na anajiunga na orodha ya watoto mashuhuri wenye majina ya kipekee.

**Zilizotrend kumuhusu**

Mnamo Agosti 2023, Khaligraph Jones alizua mzozo baada ya kuachia wimbo wa diss uliokuwa ukiwalenga marapa wa Tanzania. Hii ilisababisha upinzani kutoka kwa wasanii wa rapa wa Kitanzania akiwemo Rosa Ree, Msodoki Young Killer na Motra The Future. Mwanamuziki wa Bongo, Harmonize, ambaye Khaligraph aliwahi kushirikiana naye hapo awali pia aliingia kwenye mzozo huo kulaani kutoheshimiwa kwa wasanii wa Tanzania.

Lakini baadae Khaligraph Jones aliomba radhi kwa wanamuziki wa na kueleza majuto kwa kuwaingiza kwenye mgongano wa kimuziki usiokuwa wa lazima.

Pia mwanamuziki huyo anayejiita rap OG alianza kwa kukiri kwamba maneno yake yalitolewa nje ya muktadha na hivyo kusababisha uhusiano wake na wanamuziki wengine. Khaligraph alisema hakuwa na jinsi zaidi ya kusimama kwa







## Kona ya Urembo

Na Hidaya Machuppa Simu: +255 765 828 219

# Jinsi ya kufanya nywele zako ziwe na afya, asili na nzuri

KUWEKA nywele zako kwa afya na maridadi kwa wakati mmoja inaweza kuwa kitendo cha kusawazisha. Kwa mbinu sahihi, unaweza kuweka mwonekano wako wa asili na mzuri bila tani ya bidhaa za kupiga maridadi kila siku. Soma baadhi ya vidokezo hivi ili kubadilisha tabia zako za urembo na kufanya nywele zako ziwe za kushangaza!







**1.Usichane nywele zako zikiwa zimelowa.**

Kuchana nywele wakati mvua inaweza kusababisha uharibifu kwa nywele zako. Kabla ya kuingia kwenye oga, chukua brashi au chanuo lenye meno mapana na uanze Kuchana mwisho wa nywele zako.

Zungusha kwa upole na uelekeze juu kuelekea kichwa chako, ukiwa mwangalifu usivute au kuvuta nywele zako unapoenda.

Ikiwa una nywele za curly, unaweza kusubiri hadi baada ya kuoga na kuchana nywele zako zikiwa na unyevu na kuchana kwa meno mapana.

**2.Oga kwa maji ya joto, sio moto.**

Maji ya moto huondoa mafuta yako ya asili kutoka kwa nywele zako. Kwa bahati nzuri, sio lazima kuoga maji baridi ya barafu, pia! Punguza halijoto ya maji yako hadi maji yawe ya joto, lakini yasiwe na joto kali. Itasaidia kulinda nywele zako na kuzuia kukauka sana baada ya kuosha.

Joto bora zaidi ni chini ya 112 °F (44 °C). Ikiwa kuoga kwako kunavukiza, labda ni moto sana.

**3.Tumia bidhaa ambazo hazina silikoni na salfati.**

Viungo hivi vinaweza kukausha nywele zako. Unaponunua shampoo na kiyoyozi, tafuta chupa zinazosema "silicone- na sulfate-free" juu yao. Hawatakausha nywele zako sana, na utaweka mafuta yako ya asili zaidi kwenye kichwa chako.

Pia epuka bidhaa zilizo na pombe ndani, kwani zinaweza kukausha nywele zako pia.

**4.Weka shampoo yako kichwani.**

Hakuna haja ya kupata shampoo juu ya kila kamba ya nywele. Unapokuwa katika kuoga, weka nywele zako na kuweka glob ya shampoo mikononi mwako. Paka shampoo kwenye kichwa chako, na utumie vidole vyako kukanda bidhaa kwa upole kwenye nywele zako.

Unapoosha, shampoo itashuka hadi mwisho wa nywele zako na uhakikishe kuwa ni safi kabisa.

Kuweka shampoo moja kwa moja kwenye ncha za nywele kunaweza kukauka na kusababisha uharibifu. Zaidi ya hayo, mwisho wa nywele zako ni mara chache sana chafu au greasi.

Ingawa inaweza kujisikia vizuri, jaribu kuepuka kishawishi cha kukwaruza kichwa chako kwa kucha unapotumia shampoo. Hii inaweza kuharibu kichwa chako na kusababisha masuala kama vile mba na muwasho.

**5.Fanya mask ya nywele mara moja kwa wiki.**

Wape nywele zako upendo wa ziada kila wiki au zaidi. Ukiwa bado katika kuoga, paka kinyago cha nywele au kiyoyozi kwenye ncha za nywele zako na uiruhusu ikae kwa takriban dakika 10.

Osha kabla ya kutoka nje ya kuoga ili kutoa nywele zako unyevu wa ziada na kuangaza.

Angalia vinyago vya nywele na viyoyozi vyenye mafuta ya parachichi, mafuta ya mizeituni au mafuta ya mizeituni ndani yake kwa ajili ya unyevu asilia.

Unaweza kutengeneza kinyago chako cha nywele kwa kuchanganya vijiko 2 (30 mL) vya mafuta ya nazi, kijiko 1 (15 mL) cha mafuta ya mizeituni, na 1/2 kikombe (120 mL) cha asali.




**6.Funga nywele zako kwa taulo.**

Kusugua nywele zako na kitambaa kunaweza kusababisha uharibifu. Unapotoka kwenye oga, punguza kwa upole maji ya ziada na uondoe nywele zako na kitambaa.

Ifungeni ili maji mengi yatoke kabla ya kuyaacha yawe kavu.

Ikiwa unahisi kupendeza, jaribu kutumia kitambaa cha microfiber badala ya pamba. Wao ni mpole na husababisha baridi kidogo unapokausha nywele zako.

**7.Tumia zana za kutengeneza joto kwa uangalifu.**

Lenga mara moja kwa wiki zaidi. Vikaushio vya nywele, vya kunyoosha nywele, na vyuma vya kukunja vinaweza kukauka na kuharibu nywele zako. Unapozitumia, hakikisha unanyunyizia kinga ya joto kwenye nywele zako ili zisiharibike sana.

Jaribu kutumia mitindo ya nywele isiyo na joto, kama vile kusuka nywele zako zikiwa zimelowa ili kuunda mawimbi laini.

**8.Weka nywele zako kwa hali ya kawaida mara kwa mara.**

Ikiwa umewahi kuona kwamba nywele zako zinaonekana kuwa kavu, zipe pumziko kutoka kwa kufungwa kila wakati.

Jaribu kutumia scrunchie badala ya bendi ya nywele. Wao ni laini zaidi kwenye nywele zako na hazivuti sana kwenye kichwa chako.

**9.Kula chakula chenye uwiano.**

Lishe sahihi inaweza kukupa nywele ndefu, zenye afya. Hakikisha unakula protini nyingi konda, nafaka nzima, matunda, mboga mboga, na mafuta ya mimea kwa kiasi. Mayai, mchicha, mboga za majani, matunda na parachichi ni nzuri sana kwa afya ya nywele zako.

Ikiwa unataka, unaweza kuchukua multivitamin kila siku ili kuhakikisha kuwa unapata virutubisho vyote unavyohitaji.

**10.Vaa kofia ya kuogelea unapoogelea.**

Kinga nywele zako kutokana na kemikali kali. Unapoenda kuogelea, vaa kofia ya kuogelea na uhakikishe kuwa nywele zako zote zimefungwa vizuri chini. Unapotoka kwenye bwawa, suuza haraka ili kuepuka kukausha nywele zako na klorini.

Ikiwa una nywele za blonde, ni muhimu sana suuza baadaye. Klorini inaweza kugeuza nywele za blond kuwa kijani ikiwa imesalia kwa muda wa kutosha.

Ikiwa hujisikii kuvaa kofia ya kuogelea, osha nywele zako kwa maji safi, safi na kiyoyozi kabla ya kuruka kwenye bwawa. Maji safi yatafanya kuzuia nywele zako zisiloweke kwenye klorini au chumvi yoyote.

**11. Kata nywele kwenye ncha kila baada ya wiki 6 hadi 8.**

Kukata nywele husaidia nywele zako kuonekana zenye afya na nzuri. Nenda kwenye saluni na uchukue kidogo ili uondoe ncha za mgawanyiko na uharibifu. Ikiwa nywele zako hukua polepole, unaweza kuzisukuma hadi kila baada ya miezi 2.

Kukata nywele hakusaidii nywele zako kukua haraka, lakini husaidia ncha zako kuonekana kamili na zenye afya.


**12.Lala kwenye foronya ya hariri.**

Foronya za pamba husababisha msuguano mwingi. Unapoenda kulala, badilisha foronya yako kwa hariri au satin ili kulainisha kufuli zako unaposinzia.





Leo yetu ndiyo kesho yetu
Uelekeo Spoti
Jumamosi Desemba 09-12, 2023



# MIAKA 62 YA MAFANIKIO KATIKA MICHEZO NCHINI

**Na Mwandishi Wetu**

TANZANIA inaadhimisha miaka 62 ya Uhuru ikiwa na kicheko katika nyanja ya sanaa na michezo.

Mafanikio makubwa katika mwaka huu wa 62 yanaonekana katika mchezo wa Soka, golf na kuogelea.

Pamoja na mafanikio hayo lakini uamuzi wa Rais Samia Suluhu Hassan kuweka mkono wake katika michezo yote umeonekana kutengeneza morali kubwa zaidi kwa Wanamichezo kufanya vizuri.

Idadi ya timu ambazo zimekuwa zikishiriki mashindano ya Kimataifa imeongezeka kutokana na serikali kupitia Baraza la Michezo la Taifa (BMT) kuwezesha timu na Wanamichezo kusafiri bila wasi wasi kwa kusaidiwa nauli za safari.

Lakini si michezo tu, hata wasanii wamekuwa wakipatiwa mikopo ya muda mrefu kwa ajili ya kuboresha kazi zao na kutengeneza mfumo wa kujitegemea.

Kupitia mfuko wa Utamaduni, wasanii kutoka kada mbalimbali wamepewa mikopo kwa ajili ya kununulia vifaa, kufanya masoko na mengine mengi kuhakikisha wanaongeza kipato.

Mikopo hii yenye riba nafuu imekuwa msaada kwa wasanii hao ambao kwa namna moja au nyingine walikuwa hawawezi kukopesheka benki.

Hii ilitokana na mabenki mengi kutotambua sanaa kama kazi rasmi.

Kwa serikali kutoka mikopo ni dhahiri kuwa wametambuliwa rasmi kama ambavyo imekuwa tangu enzi za kupigania Uhuru ambapo walikuwa mstari wa mbele.

Bado serikali imeendelea kuwatumia wasanii katika shughuli mbalimbali za kitaifa na kuelimisha jamii.

Tukirudi kwenye michezo timu ya Taifa ya Kuogelea imeweza kutwaa medali za dhababu katika mashindano ya Afrika yaliyofanyika Rwanda. Wachezaji wote nane wa timu hiyo walirudi medali za dhahabu.

Timu ya Taifa ya Golf ikiwa katika mashindano ya Afrika huko huko Rwanda ikatwaa ushindi wa kwanza.

Timu ya Taifa ya soka ya Wanawake 'Twiga Stars' imeweza kukata tiketi ya kucheza michezo ijayo ya Olimpiki.

Kama haitoshi Twiga wamefanikiwa tena kukata tiketi ya Mashindano ya Mataifa ya Afrika WAFCON yatakayofanyika Morocco mwaka 2024.

Kaka zao timu ya mwanaume wamefanikiwa pia kucheza fainali za Mataifa ya Afrika mwaka 2024 ambazo zitafanyika Ivory Coast.

Timu hizi za soka zimelamba mzigo wa milioni 200 kila moja kutoka katika kapu la mama.

Kapu la Mama lilianza kutoa motisha katika michezo ya Klabu Bingwa Afrika na Kombe la Shirikisho msimu uliopita ambapo kila goli Rais Samia alitoa sh milioni 10.

Miaka 62 imekuwa na mafanikio zaidi katika soka kwa Tanzania kuaminiwa kuandaa michuano ya Mataifa ya Afrika 'AFCON'.

Kwa kupitia PAMOJA BID, Tanzania itashirikiana na Kenya na Uganda katika kuandaa michuano hiyo mkubwa.

Wakati Tanzania kapata fursa hiyo, miaka hii 62 imeshuhudia mashindano mengine makubwa kabisa ya soka ya klabu Afrika yakifanyika Tanzania na timu ya Simba ikiwakilisha.



Lakini katika miaka hii 62 tumeshuhudia timu kutoka Mataifa ya Kongo Sudan zikiweka malazi Tanzania kwa ajili ya kutumia viwanja kwa mechi zao za Kimataifa.

Hii inadhihirisha Ubora wa miundo mbinu yetu lakini amani ambayo imetawala.

Uwepo wa mashindano katika ardhi ya Tanzania unafungua uchumi katika sekta mbalimbali ambazo zilikuwa zimedorora, mfano sekta ya hoteli na utalii.

Kipato na uchumi wa watanzania vitaongezeka zaidi kupitia michezo.

Katika miaka hii 62 ya Uhuru tumeona Idadi kubwa zaidi ya wachezaji wa Soka wa kike wakienda kucheza soka la kulipwa nje ya nchi.

Baadhi ya wachezaji hawa ni kama Opah Clement, Aisha Masaka, Julieth Singano, Enekia Kasonga, Diana Lucas, Mariam Yusuph, Anastazia Lucian na Fatuma Mwisendi.

Hii ina faida kubwa kwa wachezaji na Taifa kwa ujumla. Wachezaji wanaingiza kipato lakini serikali nayo inafaidika kutokana na kipato hicho kupitia kodi na uwekezaji unaofanywa na wachezaji hao nchini.

Kama haitoshi timu ya Taifa inafaidika na huduma kubwa ya wachezaji hao ambao wana kuwa na uzoefu wa Kimataifa.

Kwa upande wa timu ya wanaume, katika mwaka huu wa 62 timu ya Taifa ndio imekuwa na wachezaji wengi zaidi wanaoishi na kucheza Ulaya waliotamani kuchezea timu ya Taifa.

Wachezaji hao ni kama Haji Mnoga, Ben Starkie, Morice Abraham, Charles M'mombwa, Kwesi Kawawa.

Hii ni miaka 62 ya mafanikio ya michezo.



**Kapu la Mama lilianza kutoa motisha katika michezo ya Klabu Bingwa Afrika na Kombe la Shirikisho msimu uliopita ambapo kila goli Rais Samia alitoa sh milioni 10.**



## Yanga yalazimisha sare 1 - 1 na Medeama Ghana